# UFUTUHI KATIKA NYIMBO ZA SHEREHE ZA UNYAGO WA WAZARAMO: UTUMIZI NA DHIMA ZAKE KWA HADHIRA

Na

Saad Juma

Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2014

**ITHIBATI**

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo **"*Ufutuhi katika Nyimbo za Sherehe za Unyago wa Wazaramo: Utumizi na Dhima Zake kwa Hadhira",*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

……

Bw. Athumani S. Ponera
(MSIMAMIZI)

Tarehe ……

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **Saad Juma** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Shahada yoyote.

Saini……

Hairuhusiwi kunakili kutafsiri kupiga chapa au kuiga sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ridhaa ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma

**SHUKRANI**

Mosi, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kunijalia nguvu na afya njema wakati wote tangu kuanza, hadi kukamilika kwa Shahada yangu ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili.

Pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa utafiti Bw. Athumani S. Ponera kwa msaada wake usio na kifani uliowezesha kukamilika kwa tasnifu hii. Pia, ninawashukuru wahadhiri wangu wote walionilea kitaaluma katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Kwa uchache wao ni Prof. Joshua Madumulla, Prof. Lakshmanan Venkatachalam, Dkt. Elias Songoyi, Dkt Muhammed Seif Khatib, na Dkt. Rafiki Sebonde kwa kunipatia elimu thabiti ambayo ninaweza kukiri kuwa ndiyo chachu ya kukamilika kwa tasnifu hii.

Tatu, napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu wote wa Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili wa mwaka 2012-2014. Zaidi, ni wanakikundi wenzangu tuliokuwa tukijadiliana na kuwekana sawa katika masuala ya kitaaluma. Nao ni; Anakreth Kahwa, Chagaka Getruda, Kidashari Fatuma, Mgunda Madirisha, Mliawantu Felix, Mwakibete Hebron, pamoja na Sanga Edom.

Mwisho, nawashukuru wazazi wangu wapendwa Bi. Rukia H. Katundu na Bw. Juma H. Mzee. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa familia yote ya baba yangu mkubwa, Mhandisi Ally Simba na Bi. Jenipher Michael kwa kunivumilia kipindi chote cha uandishi wa tasnifu hii. Bila kuwasahau ndugu zangu Khalid Juma, Abdillahi Juma na Abubakari Juma. Wote nawathamini sana na Mungu awabariki.

## TABARUKU

Ninatabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu, **Rukia H. Katundu** na **Juma H. Mzee** ambao kwa hakika wamejitoa kwa hali na mali tangu kuzaliwa kwangu na baadaye kunisomesha mpaka kufikia hatua niliyonayo sasa.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza ujitokezaji wa ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo kwa kuangalia utumizi na dhima zake kwa hadhira. Dhana ya ufutuhi imefasiliwa kuwa ni hali furaha, ucheshi, kicheko au tabasamu itokanayo na vijenzi mbalimbali. Vijenzi vya ufutuhi vilivyomakinikiwa katika utafiti huu ni kejeli, vijembe, dhihaka, na balagha.

Utafiti ulifanyika uwandani na maktabani ambapo data za utafiti zilikusanywa na baadaye kuchambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya ufafanuzi wa kimaelezo. Maeneo yaliyotumika katika kukusanya data za utafiti yalikuwa ni mikoa ya Pwani, Dar es salaam na Dodoma. Uchambuzi wa data ulizingatia misingi ya nadharia ya Uhalisia ambayo ni; uhalisia kama mwelekeo, uhalisia kama mbinu ya kisanaa, na uhalisia kama mbinu ya kihakiki. Nadharia hii ilisaidia kufafanua uwiano uliopo kati ya sanaa ya uimbaji itumikayo katika sherehe za unyago wa Wazaramo na uhalisia wa matukio ya kila siku yatokanayo na mfumo wa maisha ya jamii hii.

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa hali ya utani, hofu na sababu za kihistoria ndizo huwafanya Wazaramo watumie tungo za kifutuhi wakati wa sherehe za unyago. Pia, matokeo yanabainisha kuwa Wazaramo hutumia ufutuhi katika nyimbo za unyago wa kama kibebeo cha fikra, na hisia zinazolengwa kuwekwa wazi mbele ya hadhira iliyokusanyika. Ufutuhi unaochopekwa katika tungo hizi huifanya hadhira kuzing’amua na kuzielewa kwa njia iliyojaa ucheshi, kicheko, na tabasamu. Dhamira hizi huweza kumhusu mwali wa Kizaramo anayefanyiwa unyago, mzazi au mlezi wake pamoja na washiriki wengine waliokusanyika katika sherehe husika.

**YALIYOMO**

**ITHIBATI** ..... **i**
**IKIRARI NA HAKIMILIKI** ..... **ii**
**SHUKRANI** ..... **iii**
**TABARUKU** ..... **iv**
**IKISIRI** ..... **v**
**YALIYOMO** ..... **vi**
**ORODHA YA VIELELEZO NA PICHA** ..... **ix**

**SURA YA KWANZA** ..... **1**
**UTANGULIZI** ..... **1**
1.1 Ufafanuzi wa Dhana ..... 1
1.1.1 Ufutuhi ..... 1
1.1.2 Dhihaka ..... 3
1.1.3 Kejeli ..... 3
1.1.4 Vijembe ..... 4
1.1.5 Balagha ..... 4
1.1.6 Unyago ..... 5
1.2 Historia Fupi ya Wazaramo ..... 6
1.2.1 Eneo la Kijiografia ..... 7
1.2.2 Shughuli za Kiuchumi ..... 8
1.2.3 Lugha ..... 9
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti ..... 10
1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti ..... 15
1.5 Malengo ya Utafiti ..... 16
1.5.1 Lengo la Jumla ..... 16
1.5.2 Malengo Mahsusi ..... 16
1.6 Maswali ya Utafiti ..... 16
1.7 Umuhimu wa Utafiti ..... 16
1.8 Nadharia ya Utafiti ..... 17
1.9 Hitimisho ..... 19
**SURA YA PILI** ..... **21**
**MAPITIO YA MAANDIKO** ..... **21**

2.1 Utangulizi ..... 21
2.2 Machapisho kuhusu Nyimbo ..... 21
2.3 Machapisho kuhusu Unyago ..... 26
2.4 Mapengo Yanayojitokeza ..... 31
2.5 Hitimisho ..... 31

**SURA YA TATU ..... 32**
**MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI ..... 32**
3.1 Utangulizi ..... 32
3.2 Mpango wa Utafiti ..... 32
3.3 Eneo la Utafiti ..... 32
3.4 Walengwa wa Utafiti ..... 33
3.4.1 Jamii ya Watafitiwa ..... 33
3.4.2 Usampulishaji na Sampuli Iliyotumika ..... 34
3.5 Ukusanyaji wa Data ..... 35
3.5.1 Njia Zilizotumika wakati wa Ukusanyaji Data ..... 35
3.5.2 Zana Zilizotumika Wakati wa Ukusanyaji wa Data ..... 36
3.5.3 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake ..... 37
3.6 Uchambuzi wa Data ..... 37
3.7 Changamoto Zilizojitokeza katika Utafiti Huu ..... 38
3.9 Hitimisho ..... 40

**SURA YA NNE ..... 41**
**MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ..... 41**
4.1 Utangulizi ..... 41
4.2 Miktadha Inayozungukia Nyimbo za Sherehe za Unyago wa Wazaramo ..... 41
4.2.1 Utani ..... 43
4.2.2 Haja ya Kuwafumbia Mahasimu ..... 43
4.2.3 Kuendeleza Historia ..... 44
4.3 Tungo za Kifutuhi Zinazojitokeza katika Nyimbo za Unyago wa Wazaramo ..... 46
4.4 Dhima za Ufutuhi katika Nyimbo za Sherehe za Unyago wa Wazaramo ..... 73
4.4.1 Kudokeza Mawazo Mazito ya Mwimbaji kwa Hadhira ..... 74
4.4.2 Sanaa ya Kufunda Mwali wa Kizaramo ..... 75

4.4.3 Nyenzo ya Kuendeleza Usemezano ..... 76
4.4.4 Sanaa ya Kuburudisha Hadhira ..... **77**
4.4.5 Kitambulisho cha Jamii ya Wazaramo ..... **78**
4.5 Hitimisho ..... 78

**SURA YA TANO ..... 80**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 80**
5.1 Utangulizi ..... 80
5.2 Muhtahsari wa Tasnifu ..... 80
5.3 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika ..... 82
5.4 Mambo Mapya Yanayoibuliwa na Tasnifu Hii ..... 83
5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ..... 85
**MAREJELEO ..... 87**
**VIAMBATISHO ..... 90**

## ORODHA YA VIELELEZO NA PICHA

Kielelezo: Ramani Kuonesha eneo Wanapopatikana Wazaramo ..... 8
Mwali wa Kizaramo akisindikizwa na shangazi yake wakati wa sherehe ya unyago.93
Utamaduni wa kupeana zawadi wakati wa sherehe za unyago wa Wazaramo. ..... 94
Wali wa Kizaramo wakiwa wamewekwa chini kwa ajili ya kupewa zawadi wakati wa sherehe za unyago. ..... 95
Wali wa Kizaramo wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa sherehe za unyago. . 96

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

Bi - Bibi

Bw - Bwana

CD - *Compact Disc*

Dkt - Daktari

DTV- *Dar es Salaam Television*

EATV- *East African Television*

ITV - *Independent Television*

M.A - *Master of Arts*

PhD - *Doctor of Philosophy*

Prof - Profesa

TATAKI - Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

TBC - *Tanzania Broadcasting Cooperation*

TPH - *Tanzania Publishing House*

TUKI - Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

TV- *Television*

UKIMWI - Upungufu wa Kinga za Mwili

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

Sura hii inatoa utangulizi wa jumla wa utafiti huu. Mtafiti ameanza kwa kutoa ufafanuzi kuhusu dhana mbalimbali ambazo zilitumika katika utafiti huu. Pia, amefafanua historia fupi ya Wazaramo, usuli wa tatizo, tamko la tatizo, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti.

## 1.1 Ufafanuzi wa Dhana

Sehemu hii inaelezea dhana muhimu zinazohusiana na utafiti huu. Dhana hizo ni ufutuhi, vijembe, kejeli, dhihaka na balagha.

### 1.1.1 Ufutuhi

Ufutuhi ni kipengele kimojawapo cha kisanaa ambacho huipamba kazi yoyote ya fasihi. Ponera (2010:14-15) anafafanua dhana ya ufutuhi kuwa ni neno lililopatikana kutokana na kupanuka kwa maana-msingi ya dhana ya futuhi; yaani, ufurahishaji au uchekeshaji katika tamthiliya. Chimbuko la ufutuhi ni Fasihi Simulizi ambayo ina mfungamano wa moja kwa moja na kuwepo kwa binadamu hapa duniani. Anazidi kufafanua kuwa; popote alipo binadamu, hutawaliwa na kaida za kifutuhi. Hii ndiyo sababu hasa vipengele kama utani, kejeli, dhihaka, mafumbo na vijembe hutumiwa katika miktadha mbalimbali ya wanadamu.

Senkoro (1982:29) anafafanua dhana ya ufutuhi akiihusisha na komedia. Anasema kuwa, hizi ni kazi za fasihi ambazo, kinyume na tanzia, huwa na ucheshi tangu mwanzo hadi mwisho. Kutokana na ucheshi huo, maudhui ya kazi hizo yanajengeka. Mara nyingi, ucheshi katika komedia hutokana na matumizi ya lugha ichezeayo

maneno au matukio ambayo, ijapokuwa huwa yamewekwa kikawaida, ukawaida huo umefinyangwa na wasanii kwa njia ifanyayo hadhira icheke au walau itabasamu. Anazidi kufafanua kuwa, hii ni mbinu ya kifani ambayo hutumiwa na watambaji fasihi simulizi kwa nia tofauti. Ucheshi hutumiwa kama kipumuo, hasa baada ya matukio ya kutisha, au maelezo marefu yenye kuwachosha wasikilizaji.

Matumizi ya ufutuhi yanazidi kushika kasi, na imekuwa ni njia rahisi itumikayo kufikisha ujumbe kwa jamii. Mathalani, mfumo wa kisiasa wa vyama vingi, utandawazi, na uhuru wa vyombo vya habari, vimeonekana kushamirisha mbinu hii ya kisanaa miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, wanasiasa hutumia mbinu za kifutuhi ili kutangaza sera zao kwa wananchi. Wanahabari nao, hasa wa magazeti na runinga, hutumia tungo na michoro mbalimbali iliyo katika msingi wa kifutuhi kwa ajili ya kutoa mawazo yao kuhusu masuala mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kitamaduni yanayomkabili binadamu. Baadhi ya vipindi vinavyoandaliwa kifutuhi katika vituo vya runinga ni; ‘Vituko Show kinachorushwa na Channel Ten’, ‘Orijino Komedy cha TBC’, ‘Ze Comedy cha EATV’, ‘Vunja Mbavu cha DTV’, ‘Mizengwe cha ITV’, na ‘Futuhi’, cha ‘Star TV’. Vipindi hivi huonesha viashiria vya kifutuhi vilivyojikita katika maneno na matendo ya wahusika wake, yanayowafanya watu watabasamu au wacheke. Kwa mfano, wakati mwingine wahusika wa kiume hujifanya wanawake, au wanawake kujifanya wanaume, na kubadili sauti au mwonekano ambao huleta tafakari nyingi kwa hadhira. Lakini katika uhalisia, humlenga mtu mwingine tofauti ndani ya jamii. Hutumia mbinu za kifutuhi mathalani kejeli, vijembe, dhihaka, balagha na ubeuzi ili kufafanua mambo mbalimbali ambayo yote huakisi matokeo ya mfumo wa maisha ya wanajamii.

Hali ya ufutuhi hujidhihirisha pia katika tanzu mbalimbali za fasihi hata zile zilizo nje ya utanzu huo wa tamthiliya, zikiwepo nyimbo mbalimbali za unyago, kwa lengo la kutoa ujumbe kwa njia ya uchekeshaji ama ufurahishaji hadhira. Aidha, mbinu tofauti za uimbaji, mathalani mitindo tofauti ya lugha ukiwapo ufutuhi, na utendekaji wake, huwa ni nyenzo kuu katika kubeba ujumbe kwa hadhira.

### 1.1.2 Dhihaka

Senkoro (1982:13) amefafanua dhihaka kuwa ni tamathali yenye ubeuzi mkali itumiayo maneno ambayo yanasikika vizuri masikioni wakati ambapo yamekusudiwa yatoe maana iliyo kinyume kabisa. Pia, Madumulla (2009:146) anafasili neno dhihaka kuwa ni maelezo au masimulizi yanayokusudia kubeua jambo, na hulenga kudunisha au kudhalilisha.

### 1.1.3 Kejeli

Mulokozi na Kahigi (1979:37) wanafasili dhana hii kuwa, ni usemi ambao maana yake ya ndani ni kinyume cha ukweli, na inabeua maana yake halisi; ni usemi wa kebehi ambapo kisemwacho sicho kikusudiwacho na msemaji, kisemwacho kumbe ndicho kinabeuliwa. Matumizi ya kejeli yametamalaki sana katika maisha ya kila siku ya jamii; si katika mazungumzo tu, bali pia namna wanajamii wanavyoyatoa mawazo yao katika uwanja wa mawasiliano. Kejeli hujengwa katika msingi wa msigano baina ya mawazo msingi ya wanajamii na dhana dhima halisi ya kejeli husika. Kwa upande wao, Ntarangwi (2004:106) na Madumulla (2009:147) wanaihusisha istilahi ya kejeli kuwa ni sawa na kinaya/stihizai. Wanafafanua kuwa, hii ni mbinu katika fasihi ambapo mtumiaji wa lugha hutumia maneno dhidi ya mtu au hali fulani ili kucheka na kutoa kejeli. Aghalabu, huwa ni kusema au kutenda jambo ambalo linatoa maana iliyo kinyume na vile ilivyosemwa au ilivyotendwa.

Akifafanua kuhusu dhana ya kejeli, Wamitila (2008) anasema kuwa uelewaji wa kejeli huhitaji msemaji na msikilizaji au hadhira kuwa na hisia au mwelekeo fulani kuhusu mada inayozungumzwa. Maneno ya Wamitila yana ukweli ndani yake. Hii ni kwa sababu si rahisi kwa jamii zenye utamaduni tofauti kuweza kuelewa barabara tungo za kikejeli zinazotumiwa na wanajamii. Hili linajitokeza hata katika nyimbo za unyago wa Wazaramo kwa kuwa tungo za kejeli hutumika na jamii hiyo kufikisha dhima mbalimbali ambazo hakika huakisi maisha, na matukio yatokeayo kila siku. Hivyo, ni rahisi kwa wanajamii wenyewe au majirani wanaofahamu mfumo wa maisha ya Wazaramo kuweza kuelewa kejeli zilizopo katika nyimbo hizo.

### 1.1.4 Vijembe

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004:164) inafasili kijembe/vijembe kuwa ni maneno ya mafumbo yenye kudhamiria kumsema mtu. Naye, Msokile (1992) anaelezea dhana hii kuwa ni maneno ya mafumbo au ya mzunguko yenye kumsema mtu kwa mabaya. Aghalabu, ufundi huo wa kuyasuka maneno hayo hufanywa katika namna ambayo husababisha hali ya hadhira kufurahi.

### 1.1.5 Balagha

Ni hali ya kutia chumvi ili kuongeza utamu na kuleta athari fulani (Mulokozi na Kahigi, 1979:36; Madumulla, 2009:148). Hali hiyo ya utiaji wa chumvi katika maelezo husababisha furaha ama tabasamu kwa hadhira ya kazi husika ya kifasihi, sambamba na kupata jumbe mbalimbali zilizopo katika tungo hizo.

Kutokana na fasili hizo zilizotolewa, ni dhahiri kuwa dhana zote hizo tajwa zina mwingiliano mkubwa hasa katika maana, utumizi, na dhima zake. Kwa mfano, ubeuzi mara nyingi hutumia kauli za moja kwa moja zisizo na mficho wakati kijembe hutumia maneno ya mafumbo. Kejeli, kwa upande wake, hutumia kauli za

kinyume (Kezilahabi, 1976; Senkoro, 1982 katika Ponera, 2010). Ukaribu wa dhana hizo, umesababisha dhana msingi ya ufutuhi itumike katika utafiti huu ili kuashiria maneno na matukio ya uchekeshaji au ufurahishaji katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na kutalii kwa kina utumizi na dhima zake kwa hadhira.

### 1.1.6 Unyago

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) inatoa maana mbili: Ni mkusanyiko wa vijana mahali maalum ili kufundishwa mila za kabila. Pia, ni ngoma ya kufundisha wali mila za kabila lao. Naye Bakari (2011), anafafanua dhana ya unyago kuwa ni ngazi fulani ya mafunzo yawahusuyo watoto wa kike wanaoingia katika hatua ya kuvunja ungo au katika upevu. Hutolewa ili kuwaandaa wasichana hao kuingia katika utu uzima na ili yawasaidie kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya kimwili, kiakili, kifikra na kijamii.

Dai hili limefafanuliwa zaidi na Mlama (1973) katika Omari na Mvungi (1981:161) kuwa unyago kwa ujumla ni sawa na jando; tofauti ni kwamba, unyago unashughulikia wanawake. Pia, Mhando na Balisidya (1976) wanaeleza juu ya unyago kuwa “ni kundi la sherehe kwa ujumla linalohusu kumwingiza mwanajamii kwenye kundi la aina nyingine”. Hivyo, unyago ni shughuli za kijadi zifanywazo na wanajamii ili kumpeleka au kumwondoa mtoto wa kike kutoka kundi moja la jamii na kumpeleka kundi jingine na kufundishwa kwa njia ya kisanaa ikiwemo nyimbo. Dhamira kuu ya unyago ni kumfinyanga mtoto wa kike kuwa mtu mzima, hasa kumfanya ayatambue maisha ya ndoa pindi atakapoolewa.

## 1.2 Historia Fupi ya Wazaramo

Wazaramo ni jumla ya mchanganyiko wa makabila ya kibantu. Sehemu kubwa ya mchanganyiko huo ni Wakhutu kutoka Morogoro, katika safu za milima ya Uruguru. Mwaruka (1965) anafafanua kuwa neno "Uzaramo" linatokana na neno "Kuzalamia", na maana yake ni "Kusehelea". Hivyo, Wazaramo ni waseheleaji, yaani, watu waliotoka katika sehemu mbalimbali na kufanya masikani katika ukanda wa Pwani. Anazidi kufafanua kuwa, mabadiliko ya neno hili yametokana na sababu za kimatamshi miongoni mwa watu. Neno lenyewe hasa ni Zalamo, yaani nchi iliyosehelewa. Lakini baadaye, ikabadilika na kuwa Zaramo au pengine Zaramu.


Wazaramo hawakuwa wakazi wa maeneo yao ya sasa katika kipindi cha miaka 200 iliyopita. Walihamia katika maeneo hayo wakati wa vita na Wangoni kutoka Kusini, pamoja na Wakamba kutoka Kaskazini. Wenyeji wa kabila la Washomvi ambalo ndilo lililokuwa likiishi maeneo ya Pwani kwa muda mrefu, walilazimika kuomba msaada kutoka kwa Pazi Kilama[1] wa kabila la Khutu ili kuja kupambana na wavamizi hao. Kiongozi huyu alisifika sana kwa werevu wake na ujasiri mkubwa katika shughuli za kuwinda tembo, simba, pamoja na kupigana vita. Hivyo, alisaidia kuwafukuza Wakamba mbali na maeneo hayo ya Pwani. Baada ya vita hivyo, Pazi Kilama alituma mwakilishi wake kwenda kwa Washomvi ili kudai malipo yake kutokana na kazi aliyoifanya. Washomvi walishindwa kutekekeleza ahadi waliyotoa. Hivyo, huo ndio ulikuwa mwanzo wa Pazi Kilama kuweka masikani yake ya kudumu katika maeneo hayo tangu wakati huo hadi hivi sasa.

[1] Kiongozi wa Wazaramo aliyepata umaarufu mkubwa kutokana na ushupavu wake katika kupigana vita.

Jina la Pazi ni maarufu, na kwa sasa ndilo linalounganisha koo nyingi miongoni mwa jamii hii ya Wazaramo. Koo hizi hupatikana zaidi katika maeneo ya Kisiju, Mkuranga na Maneromango. Umaarufu wa Pazi Kilama ulianzia katika kijiji cha "Mkamba", kilichopo katika wilaya ya Mkuranga, ambacho kihistoria, ndipo palipokuwa na vita vikali kati ya jeshi lake na Wakamba. Vita hivyo vilisababisha kuuwawa kwa kiongozi mkuu wa jeshi la Wakamba. Matamshi hayo ya sasa yanatokana na tofauti za kimatamshi miongoni mwa watu, pamoja na tofauti za kimapokeo kati ya kizazi kilichopita na hiki cha sasa. Hapo awali, mahali hapo palijulikana kama "Akufilile Kamba", kwa maana ya "Alipofia Mkamba".

### 1.2.1 Eneo la Kijiografia

Jamii ya Wazaramo hupatikana kwa kiasi kikubwa katika mkoa wa Pwani. Ndani ya mkoa huu, yapo maeneo ambayo Wazaramo walifika na kulowea kwa kipindi kirefu. Pia, yapo maeneo mengine ambayo yanatamalakiwa na makabila mengine kwa mfano Wakwere na Wandengereko. Upande wa Kusini wa mkoa wa Pwani kuna mto Rufiji; na Kaskazini kuna mto Ruvu. Hivyo, katikati ya mito hii miwili kandokando ya Bahari ya Hindi, ndipo mahali walipofikia Wazaramo tangu miaka ya 1700. Kwa sasa, wameweza kusambaa tena katika maeneo mbalimbali kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi, na kuingiliana kwa watu.




Kielelezo: Ramani Kuonesha eneo Wanapopatikana Wazaramo. (Chanzo: Kitabu cha Habari za Wazaramo)

### 1.2.2 Shughuli za Kiuchumi

Tangu awali hadi sasa, Wazaramo wamekuwa wakijishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kukuza kipato chao na kukidhi mahitaji ya chakula. Shughuli za kilimo zimeathiriwa zaidi na hali ya hewa iliyopo katika maeneo ya Pwani. Kama ilivyo kwa makabila mengine, Wazaramo hujihusisha na kilimo cha mazao ya chakula na biashara, ambapo wenyeji hulima mahindi, mtama, mpunga, muhogo, mananasi, viazi vitamu na mbogamboga. Mazao haya hulimwa kutegemeana na msimu ambapo wakati wa jua kali hususani msimu wa kiangazi, shughuli za kuandaa mashamba hufanyika, na wakati wa mvua nyingi za masika ama vuli, wakulima hujihusisha na upandaji. Kwa upande mwingine, Wazaramo hujihusisha na kilimo cha korosho na nazi kama mazao makuu

ya biashara. Vilevile, hujishughulisha na ufugaji wa kuku, mbuzi na bata ili kuwa na njia mbadala za kujiongezea kipato.

### 1.2.3 Lugha

Lugha ya Wazaramo ni Kizaramo. Hii ni mojawapo ya lugha maarufu katika jamii za Watanzania. Lugha hii ina uhusiano mkubwa na lugha nyingine za Kikutu, Kidoe na Kikwere. Hii inatokana na fafanuzi mbalimbali kuhusu chanzo cha kusambaa kwa Wazaramo katika maeneo ya Pwani kuhusishwa na makabila mengine ya jirani na ukanda wa Pwani. Kwa maoni ya mtafiti kuhusu wenyeji wa Pwani, hasa Wazaramo wenyewe, inaonekana kuwa lugha hii inazidi kupoteza umaarufu wake kutokana na wenyeji kutumia zaidi lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao na shughuli nyingine za kiutamaduni. Wapo baadhi ya wenyeji, hasa wazee waishio vijijini, ambao bado wanatumia lugha ya Kizaramo. Hata hivyo, wakati mwingine nao huchanganya na maneno ya Kiswahili. Mtazamo wa wenyeji kuhusu suala hili unaafikiana na maelezo yafuatayo:

> Suala la lugha ya kuzungumza katika kabila la Wazaramo halitazamwi sana kama ilivyo kwa makabila mengine. Wakazi wengi wanajiita "Waswahili"; na hivyo kuona Kiswahili kuwa ndiyo lugha yao ya mawasiliano. Wapo baadhi ya wenyeji, hasa wazee wanaoishi vijijini kama vile Marui na Chole, hutumia Kizaramo, ingawa nao wakati mwingine hutumia maneno ya Kiswahili katika kuzungumza…[2]

Kwa kiasi kikubwa, hoja hii ina ukweli kwa sababu lugha ya Kiswahili ndiyo imeonekana ikitumika hata katika mambo ya kitamaduni, kama vile sherehe za ngoma na michezo mbalimbali inayowahusu watu wa rika tofauti. Nyimbo mbalimbali ziimbwazo katika sherehe za unyago katika jamii hii, na ambazo zimeshughulikiwa katika utafiti huu, nazo zimetumia lugha ya Kiswahili, ambayo

[2] Mahojiano kati ya mtafiti na Bw. Athumani Haruna tarehe 07/10/2013, katika kijiji cha Kilimahewa, kata ya Mkamba wilaya ya Mkuranga, mkoa wa Pwani.

kwa imani ya mtafiti, inaonekana kufahamika na wenyeji wengi zaidi, badala ya ile ya kizaramo.

### 1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Unyago katika kabila la Wazaramo huchukuliwa kuwa ni mwendelezo wa mifumo ya malezi na maadili ayapatayo mtu tangu anapozaliwa hadi anapokuwa mtu mzima. Unyago huenda sambamba na jando kwa upande wa wavulana, isipokuwa unyago hulenga kufunza wasichana amali kama vile uvumilivu, kutunza siri za utu uzima, malezi ya watoto, maisha katika ndoa pamoja na heshima. Kama ilivyo kwa makabila mengine ya Kiafrika, jamii ya Wazaramo ilikuwa na mkusanyiko mkubwa mno wa ngoma za asili; hata yawezekana ikawa ni moja kati ya jamii zenye idadi kubwa ya ngoma nchini Tanzania. Ngoma hizo hasa huchezwa nyakati za sherehe kama vile harusi, unyago, na jando kwa wavulana ambapo mangariba hucheza ngoma ya msewe na sherehe nyingine kadhalika katika kutekeleza kazi yao.

Baadhi ya ngoma za Wazaramo zina mgawanyiko wa tofauti za watu, umri na jinsia. Umri wa vijana wadogo, watu wa makamo, wazee, wanawake, na wanaume, kila moja huwa na ngoma yake pamoja na namna yao ya kucheza. Mathalani, ngoma za ‘Mkole’ na ‘Msondo’ ni maalum kwa wanawake. Vilevile, kuna ngoma za mjumuiko wa jinsia zote na umri wowote. Ngoma za namna hii ni nyingi mno na ndizo zibebazo furaha ya Wazaramo. Sherehe nyingi za unyago wa Wazaramo huambatana na ngoma, hasa mdundiko. Kama ilivyo kwa makabila mengine, Wazaramo wana taratibu mbalimbali za malezi kwa watoto wao. Wanawake ndio wenye jukumu kubwa la kulea watoto wadogo. Ni nadra kukuta baba amekaa na watoto wake wadogo na kuongea nao kuhusu masuala ya kimaisha. Hata hivyo, wapo wanaume

wachache wanaofuata maisha ya kisasa kwa kukaa na watoto wao ili waweze kujua tabia na mienendo ya makuzi yao. Hufanya hivyo ili kujenga jamii yenye usawa wa kijinsia na kuwapatia watoto haki ya kukaa na wazazi wa kiume. Watoto wanapokuwa wakubwa, wazazi hugawana majukumu ambapo kina mama huwafundisha wasichana juu ya majukumu ya kutunza familia.

Msichana wa Kizaramo anapovunja ungo, huwekwa ndani ya nyumba ili kualikwa[3]. Tukio hilo huenda sambamba na kufanyiwa sherehe maalumu ya majumuisho ya kuvunja ungo ijulikanayo kama 'galigali' ambayo hutumika hasa katika kuwacheza unyago wasichana na wavulana walio kumbini au jandoni. Hii inaweza kufanywa siku hiyo hiyo au siku chache baada ya kuvunja ungo. Baada ya kufanyika kwa sherehe hii, mwali huwekwa ndani kwa miezi kadhaa au pengine mwaka mmoja au zaidi. Wakati huo wote mwali haruhusiwi kuongea kwa sauti ya kusikika. Pia, hujifunika shuka moja tu kiunoni na kuacha kifua wazi. Baba na wanaume wengine, isipokuwa kaka wa mwali hawaruhusiwi kumwona mwali. Na kama ameposwa, mchumba wake pia haruhusiwi kumwona mpaka siku ya harusi. Wakati huo wote, mwali hupata mafundisho mbalimbali kutoka kwa kungwi ambaye huitwa Mng'hunga. Mafundisho hayo yanaweza kuwa kwa njia ya nyimbo, mazungumzo ya kawaida au njia ya vitendo.

Tofauti na hivi sasa, hapo zamani wasichana wengi wa Kizaramo hawakuweza kupata fursa ya kwenda shule. Hivyo, ilikuwa ni jambo la kawaida kwa wali wa Kizaramo kuwekwa ndani kwa muda mrefu kabla ya kufanyiwa sherehe za unyago. Bi Asha Sefu anashadidia hili kwa kusema:

[3] Katika tasnifu hii, neno hili limetumika kumaanisha mafunzo maalumu anayopewa mtoto wa kike kuhusu masuala ya utu uzima

> Miaka ya zamani wakati tukiwa wadogo, ilikuwa ni lazima kwa mtoto wa Kizaramo kukaa ndani kwa muda mrefu. Miaka mitatu ilikuwa ni ya lazima kwa msichana kukaa ndani ili akue kiakili na kuwa na fikra za utu uzima. Pia, ajifunze heshima kwa kila rika, na kwa mume wake pindi atakapoolewa. Baada ya miaka mitatu kupita, kufanyika ama kutofanyika kwa sherehe ya unyago kulitegemea zaidi kipato cha mzazi au kupatikana kwa mavuno ya kutosha katika msimu huo…[4]

Baada ya miezi michache, mwali hupelekwa kwa kungwi wake kwa muda usiopungua miezi sita. Wakati mwali anapoishi kwa kungwi wake, wazazi hutayarisha sherehe inayohusu mafunzo ya mkole. Maandalizi ya sherehe hufanywa kwa kusambaza taarifa kwa ndugu na majirani kuhusu matarajio ya kuwepo kwa sherehe ya unyago katika kipindi fulani kilichopangwa. Familia hutumia kati ya miezi saba mpaka kumi ili kufanya maandalizi ya sherehe hiyo. Taarifa ya mwisho ya kuwepo kwa sherehe ya unyago hutolewa siku ya Ijumaa ya wiki ya sherehe. Hii hutolewa kwa kupiga ngoma maalumu iitwayo "mbiga" au "kibiga". Ngoma hii hupigwa mchana kwa malengo makuu mawili; kwanza, ni kiashiria cha kuanza rasmi kwa sherehe, na pili hutumika kama mwaliko kwa wote ambao kwa bahati mbaya hawakuweza kupata taarifa za kuwepo kwa sherehe ya unyago katika ukoo au familia hiyo. Siku ya kuadhimisha mafunzo haya, mwali hupelekwa mkoleni wakati wa alasiri, ambapo huko, ngoma hupigwa sambamba na waimbaji wa kike kuimba nyimbo mbalimbali za unyago.

Mkole ni mti mkubwa ambao wali wa Kizaramo hupelekwa na kuwekwa chini yake kwa ajili ya kupewa mafundisho ya unyago. Hapo awali mti huu ulitafutwa popote ulipo ili uweze kutumika kufanikisha zoezi hilo. Katika mazingira mengine ambapo

[4] Mahojiano kati ya mtafiti na Bi Asha Sefu katika kijiji cha Boga, wilayani Kisarawe tarehe 07/10/2013

mti huu haukupatikana, Wazaramo waliweza kutafuta angalau tawi moja la mti huu na baadaye kulipeleka katika eneo lililopo jirani na makazi ya watu ambapo tukio hilo limepangwa kufanyika. Katika eneo hilo, tawi hilo la mti huchimbiwa aridhini na kisha, mabinti wa Kizaramo wanaochezwa unyago huwekwa chini ya tawi hilo ili kupata tafsiri ya neno "mkoleni", na hapo shughuli za mafundo ya siri hutolewa kwa kwa njia ya nyimbo au matendo ya makungwi.

Utafiti huu haukushughulikia nyimbo hizo za siri ziimbwazo wakati wa mkole, kwani tukio hilo huwahusu akina mama na wasichana ambao wameshabalehe tu. Hivyo, nyimbo zilizoshughulikiwa ni zile zihuhusuzo sherehe za unyago ambazo hadhira hupata fursa katika kuimba, kusikiliza na kutafakari ujumbe unaopatikana katika nyimbo hizo.

Mtunzi wa nyimbo kama ilivyo kwa mtunzi yeyote wa kazi ya fasihi, huweza kuimarisha kazi yake katika matumizi ya lugha. Ni hodari wa maneno yaliyopangiliwa kwa utaratibu ambao huleta mguso na mnato kwa msikilizaji. Lugha iliyojaa usanifu, urazini, na umahiri, huwa ndicho chombo maridhawa cha Fasihi Simulizi kitumikacho kutoa ujumbe wa fanani, (Omary, 2009 na Khatib, 1978).

Matumizi ya tungo za kifutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo ni sehemu mojawapo ya mbinu za kifani ambazo hutumiwa na waimbaji wake kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa njia ya kipekee iliyojaa ucheshi na kuleta tafakari nyingi kwa hadhira. Kwa kawaida, kila wimbo uimbwao katika sherehe hizi huwa na dhamira yake ambayo mwimbaji huamua kuitoa katika mazingira hayo na kwa njia hiyo. Mwimbaji hana budi kuwa anaufahamu fika utamaduni na historia ya jamii

ambamo yale ayaelezayo yametoka. Hupaswa kuwa mzoefu wa mila na jadi anazoziibua katika maudhui ya nyimbo anazoziimba.

Mwimbaji huyo hatakiwi kuwa na aibu, bali awe mtu mchangamfu mwenye kuifurahia kazi anayoifanya ili kuifanya hadhira kujenga usikivu wa kazi hiyo, na hatimaye kuyapata maudhui yake. Pale anapohitajika kuweka madoido, sharti afanye hivyo, na pale inapombidi kutumia maneno ambayo katika muktadha mwingine yangekuwa ni matusi, hapaswi kuona aibu kufanya hivyo.

Wachunguzi na wahakiki mbalimbali wamejaribu kushughulikia masuala ya ufutuhi pamoja na nyimbo kwa namna mbalimbali. Ponera (2010), katika utafiti wake, amefafanua “Athari za Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa, na Athari Zake kwa Wasomaji”. Utafiti wake umejaribu kutalii suala la ufutuhi kwa kujikita katika fasihi andishi, hususani, nathari. Vipengele vya kifutuhi vikiwemo kejeli, ubeuzi, dhihaka na vijembe vimeonekana kuwa na mchango mkubwa katika kuleta athari kwa wasomaji. Pia, Salinguji (2011) amejaribu kuonesha “Nafasi ya Mwanamke katika Nyimbo za Wasukuma”. Utafiti wake umefanikiwa kubainisha dhamira zilizopo katika nyimbo za Wasukuma kwa kumtazama mwanamke. Ijapokuwa fafanuzi za wahakiki hawa zimegusia pande zote mbili za kihakiki; yaani, kifani ikihusisha “Ufutuhi katika Nathari”, na kimaudhui ikihusisha “Nafasi ya Mwanamke katika Nyimbo”, bado kumekuwepo na haja ya utafiti huu kwenda mbele zaidi kwa kuitazama sanaa ya ufutuhi katika Fasihi Simulizi, na kufafanuliwa zaidi kwa kutumia nyimbo za sherehe za unyago katika jamii ya Wazaramo.

Mtunzi wa kazi yoyote ya kifasihi hana budi kuibua dhamira ambazo zitaleta athari kwa hadhira yake; iwe kwa njia nyoofu au tafakari. Matumizi ya lugha kisanaa, yana nafasi kubwa katika kuifanya hadhira ing'amue mawazo ya msanii kwa kupitia tungo bunilizi zilizopo katika kazi yake. Wazaramo ni wajuzi wa kutumia lugha katika mikusanyiko ya sherehe. Nyimbo ziimbwazo katika sherehe za unyago hutawaliwa na vijembe, kejeli, dhihaka na balagha, ambavyo ndivyo vilivyojadiliwa kwa kina katika utafiti huu ili kubaini dhima zake kwa hadhira.

### 1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti

Nyimbo za unyago ni sehemu ya tamaduni za jamii; ambapo kwazo jamii hujifunza mambo mengi kupitia maudhui yaliyojificha kwenye tungo zake. Tahakiki na tafiti za wataalamu mbalimbali kama vile Bakari (2011) zimejikita katika kipengele cha kimaudhui, na kuonesha kuwa jamii nyingi za Kitanzania hutumia nyimbo kama nyenzo ya kuburudisha na kusawiri maisha ya watu ya kila siku. Wasanii wa nyimbo wamekuwa wakitumia ufundi mkubwa katika kuchagua maneno wakati wa uimbaji. Maneno hayo ndiyo hubeba mawazo ya msingi ya watunzi au waimbaji hao na kuifanya hadhira ing'amue mawazo hayo kwa njia ya burudani kulingana na muktadha huo. Aidha, ufutuhi, ni sanaa mojawapo katika uimbaji inayotumiwa sana na jamii ya Wazaramo ili kubeba ujumbe ambao mara nyingi huonekana kusawiri maisha yao ya kila siku. Ijapokuwa ufundi huu wa uimbaji umekuwepo hata katika jamii nyingine za Kitanzania, bado sanaa hii ya utumizi wa lugha, hasa katika Fasihi Simulizi, haijahakikiwa na kutafitiwa vya kutosha. Hivyo, utafiti huu unatarajia kuziba mapengo yoliyojitokeza hapo awali kwa kuzichunguza tungo za kifutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, ukijikita katika kuvitalii

vipengele vya kejeli, vijembe, dhihaka na balagha, na baadaye, kubainisha dhima zake kwa hadhira.

## 1.5 Malengo ya Utafiti

### 1.5.1 Lengo la Jumla

Utafiti huu ulilenga kuchunguza ufutuhi (hasa vipengele vya kejeli, vijembe, dhihaka na balagha) katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, muktadha na dhima za ufutuhi huo.

### 1.5.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi yaliyoongoza utafiti huu ni:-

a) Kubainisha miktadha tofauti inayowasukuma Wazaramo kutumia tungo za kifutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago;
b) Kuzichambua tungo za kifutuhi zilizopo katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na;
c) Kubainisha dhima za ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo.

## 1.6 Maswali ya Utafiti

a) Katika miktadha ipi watambaji wa nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo hutumia tungo za kifutuhi?
b) Tungo zipi za kifutuhi hujitokeza katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo?
c) Tungo za kifutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo zina dhima gani kwa hadhira?

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Kukamilika kwa utafiti huu ni hidaya kubwa kwa wadau wa Fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu umewezesha kupatikana kwa tasnifu inayotarajiwa kuleta tija

zifuatazo; Mosi, kubainisha misingi mbalimbali ya utumizi, na dhamira za ufutuhi uliopo katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na hivyo kuifanya hadhira kupata ufahamu zaidi juu ya misingi hiyo. Pili, kuimarisha juhudi za kuzilinda na kuzienzi tamaduni za Waswahili hususani tamaduni zihusuzo nyimbo za unyago. Tatu, kuhamasisha na kuwasaidia walimu na wanafunzi mbalimbali walio vyuoni, hususan, walio katika fasihi kupata uelewa kuhusu dhana na dhima ya ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo na jamii nyingine za waswahili, na mwisho, kuwasaidia watafiti wajao kupata mwongozo thabiti wa kufanya tafiti zaidi, kwa kuzingatia mapendekezo mbalimbali ya mtafiti, kuhusu mambo ambayo hayajashughulikiwa katika utafiti huu.

### 1.8 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia. Hivyo, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake umefanywa kwa kuzingatia dhana msingi ya uhalisia.

Ntarangwi (2004:48), anasema kwamba uhalisia ni uwakilishi wa mambo katika fasihi. Mhalisia huamini katika matokeo ya mambo, na ukweli unaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba. Kazi yoyote ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli na halisi.

Uhalisia ni nadharia yenye kuelezea aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambalo kazi za fasihi zinachukuliwa kama zinahifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Kimsingi, kazi za kifasihi zinatarajiwa kuwa kama akisio la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Katika mawanda ya fasihi, uhalisia hutokana na

matatizo yanayowakabili watu. Matatizo haya ndiyo yale yaliyowafanya wasanii kuutuhumu ulimbwende ambao matamanio yake yalikuwa ni ya kinjozi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu (Wamitila, 2002; Wafula na Njogu, 2007).

Kufikia mwaka 1798, wahakiki kama vile Schiller walikuwa wakitumia dhana mbili za udhanifu na uyakinifu kuashiria vinyume. Kutokana na historia hii, dhana ya uhalisia imekuja kuhusishwa na miktadha miwili: Wa kwanza, ni ule unaoitazama kama njia ya kutathmini hali. Huu huhusisha uhalisia wa maisha ya watu. Wa pili, unaitazama dhana hii kama kazi ya sanaa inayoonyesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo, kwa kuhusianisha na uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu kwa kutumia mbinu za kisanaa.

Nadharia hii iliwekewa misingi yake na mwanafalsafa aliyejulikana kama G. F Hegel, katika kitabu chake kilichojulikana kama *Aesthetics*, Ujumi (1886). Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno “Uhalisia” kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inawasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii (Wamitila, 2002). Wakizungumzia juu ya suala la Uhalisia, Wafula na Njogu (2007:62-63) wanasema, istilahi ya uhalisia imediriki kuhusishwa na mikondo mitatu: Mosi, ni uhalisia kama Mwelekeo. Katika mkondo huu, uhalisia ni mwelekeo unaozingatia njia za kisayansi kutekeleza jambo. Pia unasisitiza upinzani dhidi ya mtazamo wa kinjozi juu ya maisha, na kupingana na ulimwengu. Pili, uhalisia kama mbinu ya kisanaa. Katika mkondo huu, uhalisia unahusishwa na mbinu iliyo na mashiko katika hali halisi ya maisha ya watu na uwezo wa kuonesha hali ya kisaikolojia ya watu. Na tatu, uhalisia kama mbinu ya Kihakiki. Katika mkondo huu, wataalamu hawa wanasema, uhalisia huzingatia

muundo na muwala katika kazi ya fasihi. Aidha, huutazama uchambuzi wa kazi ya sanaa kama zao linalojitosheleza. Hili, hufanyika kwa kuihusisha hali halisi ya wahusika na lugha wanayotumia, na mwishowe, kuainisha vielelezi vya kihistoria vinavyosababisha mabadiliko makubwa ya kijamii.

Kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa kazi za kifasihi hukusudia kusawiri jamii katika matukio halisi ya kila siku kwa njia ya kisanaa. Tungo za kifutuhi ni sehemu ya vipengele vya kifani katika kazi yoyote ya kifasihi, ambayo dhima yake kuu ni kubeba ujumbe unaoisawiri jamii katika matendo halisi yaliyopo au yatokeayo. Aidha, utafiti huu umejaribu kuzitalii tungo za kifutuhi zenye kejeli, vijembe, dhihaka, ubeuzi na balagha, katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na kubainisha dhima zake katika kusawiri na kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha.

Kimsingi, mikondo mikuu inayofafanua nadharia ya uhalisia, imedhihirika kwa uwazi katika tasnifu hii. Nadharia hii ilikidhi haja kuu ya utafiti; yaani, kuchunguza matumizi ya ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na kubainisha dhima zake kwa hadhira. Kwa kiasi kikubwa, uchambuzi na uwasilishaji wa data zetu ulifanywa kwa kuzingatia mikondo miwili; ambayo ni ule unaoutazama uhalisia kama mbinu ya kisanaa, na uhalisia kama mbinu ya kihakiki.

### 1.9 Hitimisho

Kwa ujumla sura hii imetoa utangulizi wa jumla wa utafiti ambapo dhana teule zimefafanuliwa, maswali, umuhimu na nadharia ya utafiti. Aidha, katika sura

inayofuata mapitio ya maandiko yamefanyika kwa kuzingatia fafanuzi zilizopo katika sura hii**.**

## SURA YA PILI

## MAPITIO YA MAANDIKO

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusisha maandiko au machapisho ambayo yanahusiana na mada hii. Inadokeza jinsi wataalamu na watafiti mbalimbali walivyotoa mawazo yao kuhusu nyimbo za sherehe za unyago, na dhima zake kwa jamii.

### 2.2 Machapisho kuhusu Nyimbo

Miongoni mwa tanzu za mwanzo kabisa za kifasihi ambazo zilipata kutumiwa na mwanadamu katika shughuli zake za kila siku ni nyimbo. Utanzu huu ulitumiwa kama chombo cha utamaduni wa jamii husika kwa sababu nyimbo hubeba dhima kubwa ya kuelimisha, kukosoa, kukemea na kuadilisha. Vyote hivi hufanywa kwa njia ya barudani ambapo huifanya hadhira au walengwa kuwa na furaha huku wakipata maudhui ya nyimbo hizo.

Mulokozi (1996) anafafanua nyimbo kuwa ni kila kinachoimbwa. Anaeleza kuwa ni dhana pana inayoweza kujumuisha tanzu nyingine tofauti za fasihi simulizi zikiwasilishwa kwa namna ya nyimbo. Anazidi kufafanua kuwa nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii za Kiafrika. Hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kufunza, kuarifu, kunogesha hadithi, kuomboleza, kubembeleza mtoto kuchapua kazi na kutia hamasa vitani. Hivyo, anabainisha nui kuu za nyimbo kama vile tumbuizo, tukuzo, chapuzo na tenzi/tendi.

Ufafanuzi wa Mulokozi umetoa dhana ya nyimbo kwa ujumla wake; ambapo amebainisha pia kuwepo kwa tanzu tofauti za fasihi zinazoweza kuwasilishwa kwa

namna ya uimbaji. Aidha, nyimbo za sherehe za unyago ni mojawapo ya tanzu hizo ambazo pia, huwa na dhima mbalimbali kwa jamii. Hivyo, ufafanuzi wake umetoa mwongozo mzuri wakati wa kuchambua data za utafiti huu zilizohusu kipengele cha ufutuhi, kama sanaa ya lugha yenye kubeba dhamira za waimbaji wakati wa sherehe za unyago wa Wazaramo.

Balisidya (1987) anaeleza kwamba "nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, kongosio, mapigo na muwala. Nyimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja pekee ama na wazumi wake, wakiitikia Mkarara". Anazidi kueleza kuwa, nyimbo huwa na ladha kama vile vina, mlio katika takriri, tanakali sauti na mrudiorudio wa maneno. Naye Thonya (1978) anasema "Nyimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana ya ujumbe kwa jamii. Vionjo vilivyobainishwa na Balisidya katika ufafanuzi wake vina ukweli, kwa kuwa kuwepo kwake huzifanya nyimbo nyingi kuweza kuchanuza dhamira zake kwa sanaa ya burudani yanye kuvutia hadhira. Zipo fani nyingi ambazo hutumiwa na waimbaji ili kukidhi malengo ya nyimbo zao; ambapo, ufutuhi ni fani mojawapo ambayo imechambuliwa na kufafanuliwa katika utafiti huu, kwa kuvitazama vijenzi vyake vinavyojitokeza katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo.

Wafula na Ndugo (2007) wakimnukuu Frenchen (1962:321), wanasema kuwa nyimbo ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalumu. Mawazo hayo hayawezi kutolewa kwa hadhira katika mazungumzo ya kawaida yakaeleweka kirahisi au kuleta athari iliyokusudiwa. Mawazo ya binadamu husukumwa na nguvu maalumu iliyozingirwa wakati huo kama vile furaha, hofu, uchungu na hasira. Mawazo huweza kumfika mtu kichwani na kumfanya apumue

kwa mashaka na moyo kumdunda. Mwanadamu hujikuta akiathirika kwa namna fulani, halafu kunakuwa na matukio fulani mapya. Maneno yatakayohitajika katika kulieleza tukio hili jipya yatajitokeza yenyewe; na hayo ndiyo yatakayounda wimbo mpya.

Kutokana na mfumo wa kimaisha waishio Wazaramo, mambo mengi yatendekayo ndani ya jamii ni matokeo ya misukumo ya kihisia inayosababishwa na wanajamii wengine. Hapo ndipo hisia za kero ama furaha hujijenga katika nafsi za watu. Wengine huamua kubuni namna ya kuzielezea hisia hizo mbele ya hadhira. Hivyo, uimbaji wa nyimbo katika muktadha wa unyago, ni mbinu mojawapo ambayo hutumiwa na jamii hii kama njia ya kutoa mawazo yao. Hapo ndipo bunilizi za kifutuhi hutumiwa na waimbaji kama mbinu ya kisanaa inayorahisisha kubeba mawazo hayo kwa njia ya burudani.

Mazigwa (1991:36) anafafanua kuwa nyimbo ndizo zichukuazo maudhui mazito ambayo huonesha maisha yaliyomo katika jamii. Nyimbo huelimisha na kuikosoa jamii inapoelekea kuzama katika dimbwi la upotevu au wakati jamii inapoelekea kuachana na falsafa yake. Ufafanuzi wa Mazigwa una ukweli ndani yake, kwa sababu msingi mkuu wa nyimbo ni kufikisha ujumbe kwa njia ya burudani ya uimbaji. Aidha, matumizi ya ufutuhi na mbinu nyingine za kisanaa, huwa na nafasi kubwa katika kuifanya hadhira itafakari kwa kina na hatimaye kuelewa kile kilichodhamiriwa na mwimbaji.

Okpewho (1992) anakiri kuwa zipo dhima nyingi za nyimbo katika sherehe za jando na unyago, ambapo anasema nyimbo zinafanana katika dhima. Anataja aina za nyimbo kuwa ni za sherehe au za kumweka au kumsimika mfalme. Pia, zipo nyimbo za vitani, za mazishi na kadhalika. Maudhui yanayoorodheshwa ni upendo, kutukuza au kusifu pamoja na kuikosoa jamii. Pamoja na kuwepo kwa hali ya kufanana kimaudhui katika nyimbo hizo, mwimbaji pia ana nafasi kubwa katika kuyafanya maudhui hayo yaweze kuifikia na kueleweka kwa urahisi ndani ya jamii. Hivyo, ufafanuzi wa Okpewho ulitoa mwongozo thabiti katika mada ya utafiti huu; ambapo, tungo za kifutuhi zilikusanywa kutoka katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na kubainisha dhima zake katika kubeba dhamira za waimbaji.

Kwa upande wake, Mkunduge (1971) anaona kuwa nyimbo za kienyeji ni kisima kimojawapo ambacho mapokeo ya mdomo yamehifadhiwa. Ni dhahiri kwamba watu waimbapo na kucheza ngoma hawakosi kuwa na wazo la kuelezea zaidi ya furaha. Utunzi wowote ni kioo cha undani na fikra za mtunzi. Hivyo, tungo zote na matendo ya mtunzi au mwimbaji wa nyimbo, ni kiashiria cha matukio halisi yanayotokea katika jamii hiyo ambapo njia rahisi ya kuyafikisha kwa hadhira iliyopo ni kupitia nyimbo. Ufafanuzi wa Mahundi (2012) unaunga mkono dai hili. Yeye anaelezea kuwa nyimbo ni kipera cha ushairi katika utanzu wa fasihi simulizi ambacho msanii hukitumia kwa lengo la kufikisha ujumbe mahsusi kwa wahusika. Katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa, msanii mara nyingi hutumia vipengele mbalimbali vya lugha kama vile tamathali za semi, taswira na matumizi mengine ya lugha. Hivyo, katika utafiti huu mtafiti aliangalia matumizi ya ufutuhi unaojitokeza katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo.

Songoyi (1989), alifanya utafiti wake juu ya mchango wa Sanaa katika Tanzania, *The Arts and State in Tanzania.* Katika utafiti wake, alijikita katika kushughulikia kazi za wasanii wawili ambao ni Kalikali na Mwinamila, hasa katika muktadha wa utendaji. Alibaini kuwa nyimbo hizo zina mchango mkubwa katika kuitazama jamii na shughuli zao katika za kila siku. Anaendelea kufafanua zaidi kuwa, jamii inapokea mabadiliko katika nyanja za kimaisha mathalani kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Mabadiliko haya yanachagizwa na sanaa za kifasihi, hasa ngoma. Utafiti wa Songoyi umefafanua maudhui yaliyopo katika nyimbo za wasanii hao. Aidha, kutokana na malengo ya mtafiti, kipengele cha fani hakijafafanuliwa kwa kina kama nyenzo ya kufikisha maudhui hayo. Utafiti huu unakusudia kukitalii kipengele hicho, ukijikita katika kuzitazama nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na kutazama dhima za tungo hizo kwa hadhira.

Masinde (2007) anafafanua falsafa ya Wabukuku na thamani yao kama inavyojitokeza katika matumizi ya lugha wakati wa sherehe za tohara. Shughuli hii inahusisha ishara na matendo kwa lengo la kuibua hulka ambazo zinaweza kuendeleza na kuhifadhi amali za jamii. Ufafanuzi huu wa Masinde unaonesha kutambua dhima ya lugha katika kuendeleza jamii. Jando ni tukio mojawapo ambalo utumizi wa lugha hupewa upekee ili kuweza kutoa maudhui kwa vijana. Aidha, suala la ufutuhi katika utumizi huo wa lugha halijafafanuliwa kwa undani katika ufafanuzi wake. Hivyo, maelezo hayo yanatoa mwongozo mzuri katika utafiti huu, kwa kukitalii kipengele hicho katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo ili kuziba mapengo yaliyopo katika fafanuzi za wahakiki na watafiti wengine.

### 2.3 Machapisho kuhusu Unyago

Waandishi na watafiti mbalimbali wamefafanua kuhusu unyago kama nyenzo mojawapo ya kitamaduni ambayo hutumiwa na wanajamii kupitishia mafudisho mbalimbali kwa vijana hasa wa kike. Mafundisho hayo hulenga kumuandaa mtoto kikamilifu juu ya maisha ya kifamilia ambayo hutarajiwa kuyaanza baada ya kuolewa.

Mfaume (2013) anaeleezea dhana na dhima ya unyago hasa kwa watoto wa kike. Katika shairi lake la "Kufunda Mwali", anaelezea faida zilizopo kwa binti aliyefundwa vema kutokana na mila za jamii Fulani. Nazo ni kufundisha uvumilivu katika ndoa, na uwezo wa kutunza mwili wake binafsi; katika ubeti wa 1 anasema:

> 1. Oneni ndoa za kale, zilivyokuwa makini,
> Hojini wazee wale, watawambia kanuni,
> Kwamba unyago ni shule, mwali hawi ujingani,
> Faida ya unyagoni, oneni ndoa za kale… (uk. 32)

Katika ubeti huu, ni dhahiri kuwa msanii amejaribu kufafanua umuhimu uliopo katika mafunzo ya unyago kwa vijana wa kike. Aidha, anasisitiza kuwa unyago ni "shule" ambayo humwezesha kijana kujitambua na kufuta ujinga alionao juu ya maisha yake ya ukubwani. Shairi hili na dhamira zake zinatoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuwa linatoa mwongozo wa kuchambua kipengele cha ufutuhi katika kubeba dhamira zilizopo katika nyimbo za sherehe za unyago, kwa kujikita zaidi katika nyimbo za Wazaramo.

Pia, katika diwani hiyo, mwandishi amejaribu kufafanua dhana ya mkole kama sehemu ya utamaduni wa Mtanzania. Katika shairi liitwalo "Na Udumishwe Mkole", anaelezea mwingiliano wa kitamaduni hasa zile za ng'ambo na hizi zetu. Tamaduni

za ng'ambo zinasababisha kudumaa kwa tamaduni zetu kwani vijana wengi hujikuta wakiiga mambo mbalimbali yaletwayo na wageni, na hivyo umuhimu wa kuudumisha mkole ni jukumu la kila mmoja. Katika ubeti wa 1 wa shairi hilo msanii anasema:

1. Mila zimetekwa nyara, fungua mboni muole,
   Ya kwetu tunayazira, ya nje ni mateule,
   Ndipo twapata hasara, twabaki kuuma ndole,
   Na udumishwe mkole, vikome vinyamkera

Pia katika ubeti wa 3 msanii anasisitiza:

3. Kigori ameupara, lakini yu na vipele,
   Basi hiyo ni ishara, hindi lina mbelewele,
   Ndege watamparura, vyema apewe mkole,
   Na udumishwe mkole, vikome vinyamkera…(uk 33)

Madondoo haya pia yanashadidia umuhimu wa kulinda tamaduni zetu huku akigusia utamaduni wa "mkole", ambayo ni mojawapo ya ngoma maarufu ya unyago wa Wazaramo. Pamoja na fafanuzi hizo, ni wazi kuwa ipo haja ya kukitazama kipengele cha lugha katika kubeba dhamira hizo. Hivyo, utafiti huu ulikwenda mbele zaidi kwa kukitalii kipengele cha ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na hatimaye, kufahamu dhima zake kwa hadhira.

Finnegan (1988) anafafanua kuwa, "Ni kawaida kwa sherehe za jando na unyago kuwa kama hatua mojawapo ya kuvuka kutoka katika hali moja ya utoto na kuingia utu uzima, na mara nyingi huwa ni kipindi cha balehe. Kwa baadhi ya jamii inaweza kuwa mapema sana na kwa baadhi ya jamii huchelewa. Kwa baadhi ya maeneo, jando na unyago hufanyika kwa watoto wenye umri kati ya miaka saba hadi minane. Shughuli hii huenda sambamba na nyimbo zinazoimbwa na watu wenye umri unaolingana kwa baadhi ya jamii. Ufafanuzi wa Finnegan umegusia masuala mawili ambayo ndiyo msingi mkuu wa kufanyika kwa sherehe za unyago. Mosi, amehusisha

sherehe za unyago kama hatua ya ukuaji kwa watoto; na pili, amegusia nafasi ya nyimbo katika kukamilisha malengo ya sherehe hizo. Maelezo haya yaliibua haja ya kufanyika kwa utafiti huu ili kukitazama kipengele cha ufutuhi, na namna tungo zake zinavyoweza kutumika na kubeba dhima mbalimbali kwa hadhira, wakati wa sherehe za unyago wa Wazaramo.

Naye, Bakari (2011) alifanya utafiti wake kuhusu athari za nyimbo za jando na unyago wa Wamakuwa kwa vijana. Katika utafiti wake, amebaini kuwa mafunzo ya jando na unyago katika jamii ya Wamakuwa yana umuhimu na dhima kubwa kwa vijana, na yanapaswa kuendelezwa. Mtafiti ameyapa mafunzo hayo madaraja tofauti kulingana na malengo yake ya kupambana na mabadiliko ya kimakuzi ya kiutu uzima. Anasema kuwa mafunzo hayo ndiyo dira ya kupatia elimu na maarifa kwa vijana juu ya stadi mbalimbali za maisha kama vile masuala ya ndoa na uzazi, malezi, nidhamu na adabu, kujitegemea, ujasiriamali, ushirikiano na mengineyo. Mtafiti anazidi kufafanua katika utafiti wake kuwa, katika miaka iliyopita, mafunzo hayo yalisimamiwa kwa uangalifu wa hali ya juu; hayakutolewa hovyo hovyo tu. Kama malengo yake yakifuatwa na kusimamiwa, vijana wa Kimakuwa watakuwa ni miongoni mwa jamii itakayokubalika katika nyanja zote kwa kuwa wameshapata stadi za maisha toka wakiwa wadogo. Utafiti wa Bakari pia umejikita zaidi katika kuchambua dhamira zilizopo katika nyimbo hizo kwa vijana. Vipengele vya kifani katika nyimbo hizo, kama nyenzo kuu katika kuchanuza dhamira, havijashughulikiwa katika utafiti wake, na hivyo kutoa msingi mkubwa katika kutafiti suala la ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo na mwishowe kubaini utumizi na dhima zake kwa hadhira.

Akifafanua kuhusu mafunzo ya unyago kwa wasichana, Kenyata (1999) anaeleza namna mabibi walivyoshiriki katika kutoa mafunzo kwa watoto wa kike katika kabila la Kimatengo. Anasema kuwa, msichana alipopata balehe, alipelekwa kwa bibi yake ambapo huko alikuwa akifundishwa mambo ya jikoni, pamoja na majukumu mengine ya mtoto wa kike mfano kukata kuni, kukoboa mahindi, kulea watoto, kumfurahisha mume wake, kutunza nyumba yake, na kujitunza yeye mwenyewe kuepukana na tabia za uhuni na umalaya. Ufafanuzi huu wa Kenyata unaonekana kushabihiana na ule wa Alfons na Daniel (2001), wanaoelezea hatua za mwanzo za utoaji mafunzo kwa vijana wa kike na wa kiume wa kabila la Wamakuwa ambazo hufanyika hata kabla ya balehe kwa watoto hao. Wanaeleza kuwa, toka zamani, Wamakuwa walikuwa wakifunza watoto wao maadili mema kifamilia yajulikanayo kwa Kimakuwa kwa jina la "*Moro wo Ncholilo*", yaani "moto wa jioni". Wanazidi kufafanua kuwa, kwa mila na desturi, vijana wadogo huwa wanatafuta kuni kwa ajili ya kuwasha moto wa jioni ili wazee wanapotoa nasaha zao wasishikwe na baridi. Nasaha za wasichana, zinahusu zaidi mafunzo ya jinsi ya kujitunza mpaka hatua ya usichana pamoja na kuwa na heshima na adabu katika jamii. Unyago hufundisha maisha ya utu uzima yenye shabaha njema ya kukataza vitendo vya zinaa kabla ya ndoa. Msichana anapovunja ungo, huwa kunakuwa na unyago mwingine unaohusu hali yake mpya. Pia, unyago huu hufundisha kuhusu usafi, heshima, jinsi mwenendo wake utakavyokuwa endapo atapata mchumba, na hatimaye maana na jinsi ya kulea mimba. Fafanuzi hizi zote, zimetoa kipaumbele zaidi katika suala la dhamira za unyago. Katika kabila la Wazaramo, tukio hilo hufungamana na sanaa ya uimbaji ambayo ndiyo iliyomshawishi mtafiti kuifafanua kwa kina, kwa kuvitazama vipengele vya ufutuhi na dhima zake kwa hadhira.

Kwa upande wake, Guwi (2003) anajaribu kufafanua kuhusu utamaduni wa jando na unyago kwa wakazi wa ukanda wa Pwani, hasa maeneo ya Kilwa. Anaeleza kwamba masuala ya jando kwa wakazi wa Kilwa huenda sambamba na unyago. Endapo familia ina mtoto wa kike na mtoto mdogo wa kiume, mtoto wa kike ndiye huanza kuchezwa unyago. Kuna mambo mengine ambayo hufanywa kwa kuzingatia taratibu za kimila. Miongoni mwayo ni tendo la mtoto wa kiume kumzunguka dada yake mgongoni mara tatu, au wakati mwingine wanaweza kuchezwa pamoja wakati atakapotolewa nje dada yake baada ya kutekeleza kunga zote za unyago. Anazidi kufafanua kuwa, unyago hauna mambo mengi kwani msichana huwekwa ndani kwa siku tatu tu. Ile siku ya kwanza huitwa *kuku juke mwali*; yaani, kumweka ndani jioni baada ya kumkamata kwa lengo la kumuweka katika hali ya utu uzima. Siku ya pili wanamtapisha kwa dawa maalumu, ambapo tendo hilo hufanywa na kungwi mkuu. Baada ya hapo, humrudisha palepale nyumbani. Siku ya tatu asubuhi ya saa 12 hadi saa 1, ndipo humtoa na kumvisha kanga mpya ikiwa ni ishara ya kukamilika kwa hatua ya kuhama kutoka katika hali ya utoto, kwenda katika utu uzima.

Maelezo hayo yanatoa ithibati kuhusu fafanuzi nyingi za wataalamu na watafiti wa masuala ya unyago, wengi wao wamejaribu kuelezea mabadiliko ya kifikra apewayo mtoto wa kike kwa kupitia mafunzo hayo. Mafunzo ambayo hutolewa kwa njia ya vitendo, maelezo ya kawaida; hususani namna mababu walivyoweza kuishi kwa furaha na kudumisha ndoa zao, au kupitia nyimbo mbalimbali. Utafiti huu ulikitazama kipengele cha nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, matumizi ya tungo za kifutuhi na kubainisha dhima zake katika kubeba ujumbe uliopo kwenye nyimbo hizo kwa hadhira.

## 2.4 Mapengo Yanayojitokeza

Maandiko yaliyodondolewa, kwa kiasi kikubwa, yanafafanua dhamira zilizopo katika nyimbo za unyago, na unyago wenyewe kama nyenzo ya utamaduni wa watu. Ijapokuwa yapo machapisho yaliyojaribu kutazama suala la matumizi ya lugha, ukweli ni kwamba yamekitazama kipengele hicho katika mwelekeo unaotofautiana na utafiti huu. Hivyo, suala la ufutuhi kama dhana msingi ibebayo kejeli, dhihaka, ubeuzi, vijembe na balagha, katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo halijashughulikiwa vya kutosha. Hali hii ndiyo iliyomshawishi mtafiti kulishughulikia na hatimaye, kuliandikia tasnifu hii.

## 2.5 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia maoni ya wataalaamu mbalimbali kuhusu masuala ya nyimbo na unyago kwa ujumla wake. Imeangalia kwa undani maana ya utanzu huu wa visasili kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Pamoja na kuwepo kwa maelezo tofauti kutoka kwa wataalamu hawa, fafanuzi zao zimekuwa ni chachu ya kuboresha fikra chanya na mtazamo wa mtafiti kuhusu mada hii. Sura ifuatayo inafafanua mbinu na vifaa mbalimbali vilivyotumiwa na mtafiti ili kukusanya, kuchambua na kuisana tasnifu hii.

# SURA YA TATU

# MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Sehemu za sura hii zanafafanua Mtafiti mpango wa jumla wa utafiti, eneo la utafiti, jamii ya watafitiwa, zana na mbinu zilizotumika, uchambuzi wa data, pamoja na vikwazo vya utafiti.

## 3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika uwandani na maktabani. Data kuhusu mada za utafiti zilikusanywa kutoka kwa watu wa jamii ya Wazaramo. Mtafiti alikwenda uwandani kwa ajili ya kuwahoji watu mbalimbali kuhusu kuwepo kwa ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, pamoja na jinsi jamii inavyoathiriwa na tungo hizo. Pia, mtafiti alikwenda maktabani ambapo maandiko mbalimbali ya wataalamu kuhusu nyimbo, uwepo wa ufutuhi, na dhima zake katika kubeba ujumbe wa nyimbo za sherehe za unyago yalipitiwa.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Pwani, Dar es Salaam na Dodoma. Maeneo yote yalihusika katika ukusanyaji wa data za uwandani na zile za kimaktaba. Uteuzi wa maeneo haya, kila moja ulitokana na sababu zifuatazo: Pwani ni sehemu ambako jamii ya Wazaramo inapatikana. Hivyo, mtafiti alipata nafasi ya kuwahoji watu mbalimbali kuhusu tungo za kifutuhi na dhima zake katika nyimbo za Wazaramo. Pia, urahisi wa kufika katika maeneo teule ya utafiti kwani mtafiti ni mkazi wa jirani

na mkoa huu. Maeneo yaliyotumika kukusanya data za utafiti huu ni pamoja na kijiji cha Kibamba, Kisiju na Kilimahewa wilayani Mkuranga, pamoja na kijiji cha Boga na Maneromango katika wilaya ya Kisarawe. Dar es Salaam na Dodoma ni sehemu zilizomsaidia mtafiti kupitia vyanzo mbalimbali vya kimaktaba kama vile ripoti za tasnifu, majarida mbalimbali na vitabu. Mtafiti alikusanya data zake katika makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pamoja na maktaba kuu ya taifa. Pia, kutokana na urahisi wa kuwapata watu mbalimbali waliowahi kuhakiki, kuandika ama kutafiti kuhusu ufutuhi kwa upande mmoja, pamoja na nyimbo za sherehe za unyago kwa ujumla wake.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni jamii ya watafitiwa na sampuli ya utafiti.

#### 3.4.1 Jamii ya Watafitiwa

Jamii ya watafitiwa ni jumla ya vitu vyote ambavyo mtafiti anaweza kuvitumia kwa ajili ya kupata data za utafiti wake. Huweza kuwa kundi la watu, eneo fulani la kijiografia, aina ya miti au aina fulani ya maandiko (Ponera, 2010:63). Hivyo, jamii iliyotumika katika utafiti huu imegawanyika katika makundi yafuatayo:

a) Nyimbo mbalimbali za sherehe za unyago wa Wazaramo. Hizi zilisaidia kuzibainisha tungo mbalimbali za kifutuhi;
b) Wataalamu mbalimbali waliowahi kushughulikia dhana za ufutuhi pamoja na dhima ya nyimbo za unyago. Hawa walisaidia kutoa mawazo yao kuhusu ufutuhi uliopo na malengo ya kuwepo kwake katika nyimbo za unyago, na,

c) Watu mbalimbali wenye ufahamu katika kuziimba, kutafsiri na kueleza ujumbe upatikanao katika tungo za kifutuhi katika nyimbo hizo.

### 3.4.2 Usampulishaji na Sampuli Iliyotumika

Mbinu ya sampuli dhamiri ndiyo iliyotumika katika ukusanyaji wa data mbalimbali za utafiti huu. Wawakilishi wachache walihusika katika utafiti badala ya wanajamii wote. Mtafiti aliwachagua wawakilishi hao kulingana na jinsi wanavyokidhi haja na malengo ya utafiti huu. Hivyo, sampuli ya utafiti huu imeundwa na makundi yafuatayo:

a) Nyimbo thelathini (30) za sherehe za unyago wa Wazaramo zenye tungo mbalimbali za kifutuhi ndani yake. Kati ya hizo, nyimbo 20 zilitumika wakati wa uchambuzi wa data. Nyimbo zote zilizoshughulikiwa katika utafiti huu zilikusanywa kutoka uwandani katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Pwani;

b) Wanawake kumi (10) waimbaji na wazazi wa kuanzia miaka arobaini, ambao, kwa imani ya mtafiti, walitarajiwa kuwa na uelewa juu ya mafunzo yatolewayo na tungo za kifutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo. Watu hawa walipatikana katika maeneo ya Maneromango na Kisiju, ambako, kwa kiasi kikubwa, jamii ya Wazaramo ambao bado wanaendeleza utamaduni wa unyago hupatikana;

c) Vijana ishirini (20) mchanganyiko wa jinsi zote (kike na kiume) miongoni mwa hadhira, ambao walihojiwa na kutoa ufafanuzi wao kuhusu dhima ya ufutuhi katika kufikisha ujumbe wa nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, na;

d) Wanataaluma na watafiti watano (05) ambao wamewahi kuandika au kuwa na uelewa kuhusu nyimbo za unyago, dhima zake na kisha kuhusianisha na matumizi ya ufutuhi katika kubeba dhima hizo.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inaeleza njia na zana mbalimbali zilizotumika kukusanya data, pamoja na utaratibu unaohusu mchakato wenyewe wa kukusanya data.

#### 3.5.1 Njia Zilizotumika wakati wa Ukusanyaji Data

Wakati wa ukusanyaji wa data, mtafiti alitumia njia kuu tatu. Njia hizo ni:-

##### 3.5.1.1 Mahojiano

Mbinu hii inahusu kubadilishana mawazo kati ya mtafiti na mtafitiwa kuhusu mada teule ya utafiti. Huweza kuhusisha mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mtafitiwa, au kwa kutumia njia ya simu (Kothari, 2004). Hii ni mbinu muhimu inayotumika sana katika tafiti zitumiazo mbinu ya ufafanuzi, kwani humsaidia mtafiti kupata taarifa za moja kwa moja toka kwa wahojiwa. Sababu ya kutumia njia hii kwa sampuli ya utafiti huu ni kutokana na kuwepo kwa tofauti katika kiwango cha uelewa na uzoefu juu ya nyimbo za Wazaramo. Mahojiano yalirahisisha ukusanyaji wa data toka kwa wanataaluma mbalimbali waliowahi kutafiti au kuandika kuhusu nyimbo za unyago. Mtafiti akiwa uwandani, alifanya mahojiano na wanawake kumi tofauti, wenye umri wa kuanzia miaka arobaini (40) au zaidi. Wanawake hawa walipatikana katika vijiji tofauti vilivyopo katika wilaya ya Mkuranga na Kisarawe, katika mkoa wa Pwani.

#### 3.5.1.2 Ushuhudiaji

Mbinu hii hutumika kukusanya data zilizopo katika hali yake ya asili. Nunan (1992) na Adewole (1984) wanasisitiza kuwa ili kugundua tabia fulani, mtafiti hana budi kuichunguza katika mazingira ya utokeaji wake. Mbinu hii ilisaidia sana kuleta matokeo chanya kwa kuwa, mtafiti alipata data za asili zisizoathiriwa kwa namna yoyote na mtafiti/mtafitiwa. Mtafiti akiwa uwandani, alishuhudia wanajamii wakicheza ngoma, huku wakiimba nyimbo mbalimbali katika sherehe za unyago zilizokuwa zikifanyika katika baadhi ya maeneo. Pia, mtafiti alilazimika kushirikiana na wanajamii aliokutana nao katika kufanya shughuli mbalimbali zilizohitajika ili kumrahisishia ukusanyaji wa data zilizohitajika katika utafiti huu.

#### 3.5.1.3 Mapitio ya nyaraka

Data za kinyaraka za utafiti huu zilikusanywa katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Maktaba Kuu ya Taifa, na maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Mbinu hii ilisaidia kupata mawazo mapya, mitazamo pamoja na nukuu mbalimbali zilizosaidia katika uchambuzi wa data za utafiti huu.

### 3.5.2 Zana Zilizotumika Wakati wa Ukusanyaji wa Data

Zana zilizotumika wakati wa kukusanya data za utafiti huu ni pamoja na; daftari na kalamu, kamera na kinasa sauti, na hojaji. Daftari na kalamu zilitumika wakati wa mahojiano na upitiaji wa nyaraka. Mtafiti alizitumia zana hizi ili kunukuu mambo muhimu yaliyofafanuliwa na watafitiwa wakati wa mahojiano. Pia, mtafiti alinukuu maandiko muhimu yaliyopo katika nyaraka mbalimbali, ambayo yalitumika wakati wa uchambuzi na uunganishaji wa data. Kamera ya kidigitali ilitumika kuchukua picha jongezi na tuli, wakati kinasa sauti kilitumika kurekodi sauti za watu

waliohojiwa ambapo picha hizo na sauti kwa pamoja vilitumika wakati wa uchambuzi wa data. Hojaji ilitumika kutoa mwongozo wakati wa mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa. Maswali yaliyoandaliwa katika zana hii, yalimsaidia mtafiti kufanya mahojiano yake bila ya kutoka nje ya malengo ya utafiti huu.

### 3.5.3 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake

Kabla ya mchakato wa kukusanya data kuanza, mtafiti aliomba ruhusa toka kwa mamlaka zinazohusika ili zimruhusu kufanya utafiti wake katika maeneo yao. Katika baadhi ya maeneo, mtafiti alitumia barua rasmi ya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ili kujitambulisha na kuomba ridhaa ya watu binafsi waliohitajika katika utafiti huu.

Data za uwandani zilikusanywa kwa kutumia njia ya ushuhudiaji, pamoja na mahojiano. Watu mbalimbali wenye uelewa kuhusu nyimbo za sherehe za unyago na kuwepo kwa ufutuhi katika nyimbo hizo, waliombwa ridhaa yao kwa mahojiano, kurekodiwa na kupigwa picha. Data za maktabani zilikusanywa kwa kutumia mwongozo wa usomaji ulioandaliwa ili kumwongoza mtafiti wakati wa kusoma tasnifu, vitabu, majarida na vielelezo mbalimbali.

Kwa ujumla data zilizokusanywa zimekidhi haja ya utafiti kwani zimetoa uwiano mkubwa na malengo sambamba na kujibu vema maswali lengwa yaliyoongoza utafiti huu.

## 3.6 Uchambuzi wa Data

Taaarifa mbalimbali za kimaudhui zilizopatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ukusanyaji data, zilichambuliwa na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti.

Malengo hayo yaliundiwa vijisehemu vidogo katika sura ya nne ili kuleta muumano wa kimaudhui na mada hii. Njia ya ufafanuzi ilitumika wakati wa uchambuzi wa data kwa kuzingatia msingi wa kihunzi cha nadharia teule iliyotumika katika utafiti huu.

### 3.7 Changamoto Zilizojitokeza katika Utafiti Huu

Mpaka kukamilika kwa utafiti huu, zipo changamoto mbalimbali ambazo mtafiti alikumbana nazo katika utafiti wake. Changamoto hizo ni kama hizi zifuatazo:

Changamoto kubwa ilikuwa ni ugumu wa kuwapata wahojiwa kwa wakati. Baadhi ya watafitiwa walipinga kuhojiwa kwa kuhofia kuwa mtafiti alikuwa katika mambo yake ya kibiashara, yaani kuwepo kwa dhamira ya kujipatia kipato kwa kuwatumia wao. Pia, wapo baadhi ya wahojiwa ambao hawakuweza kuamini haraka kama mtafiti alikuwa na nia ya dhati kukusanya data za utafiti huu, hasa nyimbo za sherehe za unyago. Baadhi yao walipohitajika kutoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya kejeli, dhihaka, vijembe, na balagha, katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, walifikiri ni suala la utani tu. Hivyo, mtafiti aliwashawishi, ikiwa ni pamoja na kuwaonesha baadhi ya kazi za wataalamu mbalimbali walizofanya kuhusu nyimbo za unyago, ili waweze kukubali kuwa mchakato huu anaoufanywa na mtafiti ni wa kawaida, na unakubalika kitaaluma.

Pia, uhaba wa fedha za kuendesha mchakato wa utafiti huu. Mtafiti alikumbana na gharama za ziada ambazo zilikwenda nje ya bajeti tarajiwa ya utafiti. Ingawa kiasi cha fedha za dharura kilitengwa katika bajeti ya utafiti huu, bado baadhi ya gharama zilikuwa kubwa kuliko fedha hizo za dharura zilizotengwa na hivyo kusababisha kuyumba kwa mtafiti kiuchumi. Kiasi cha fedha pia kilitumika kuwalipa baadhi ya

watafitiwa ambao walitoa nyimbo zao na maelezo kuhusu tungo za kifutuhi zilizopo katika nyimbo hizo. Gharama hizi pia, zilikuwa ni za ziada kwa mtafiti kwa kuwa hazikuwepo katika makadirio ya matumizi yake wakati akiwa uwandani.

Ili kupunguza na hatimaye kuepuka baadhi ya changamoto, inashauriwa kuwepo kwa mkakati maalumu wa kutoa mrejesho kwa wanajamii kuhusu tafiti mbalimbali wanazoshirikishwa na watafiti. Hili litaweza kuwasaidia wanajamii hao kufahamu kwa undani umuhimu wake. Watafiti wengi kwa sasa wamekuwa wakifanya tafiti zao kwa kuwahusisha wanajamii wa kada mbalimbali. Lakini, mrejesho kuhusu matokeo ya tafiti hizo umekuwa ukiwafikia wanataaluma pekee waliopo mashuleni, vyuoni au katika baadhi ya ofisi za idara za serikali. Serikali pia, inapaswa kuanzisha sehemu maalumu (makavazi), kuanzia ngazi za vijiji, kwa ajili ya kuhifadhi nyaraka za tafiti mbalimbali zilizofanyika katika maeneo hayo, ili wanajamii waweze kuzisoma kwa urahisi na kupata uelewa wa kutosha kuhusu mambo mbalimbali yaliyopata kutafitiwa katika jamii yao. Hili litasaidia kuleta ari na nia kwa wanajamii kuzidi kutoa ushirikiano wao kwa watafiti pindi watakapohitajika kufanya hivyo.

### 3.8 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika vijiji teule vya mkoa wa Pwani ambavyo sherehe za unyago zilikuwa zikifanyika. Vijiji vilivyotembelewa na mtafiti ni Kibamba, Kilimahewa na Kisiju vilivyopo katika wilaya ya Mkuranga, pamoja na Boga na Maneromango vilivyopo katika wilaya ya Kisarawe. Aidha, nyimbo ishirini (20) ziliteuliwa ili kubainisha namna tungo za kifutuhi (kejeli, vijembe, dhihaka na

balagha) zinavyoweza kutumika na kubeba dhamira mbalimbali za watunzi na waimbaji kwa hadhira.

### 3.9 Hitimisho

Kwa ujumla sura hii ilijikita katika kuuelezea mchakato mzima uliofanywa na mtafiti wakati wa ukusanyaji wa data huko uwandani na maktabani. Katika mchakato huo mtafiti alifanikiwa kukusanya data lengwa zilizokidhi malengo ya mada hii. Hivyo, sura inayofuata imefafanua mjadala juu ya matokeo ya utafiti ikiwa ni mwendelezo wa mchakato uliofanyika katika sura hii.

# SURA YA NNE

# MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inajadili matokeo ya utafiti. Mjadala huo umegawanywa katika sehemu tatu kulingana na malengo na maswali ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza inajadili miktadha mbalimbali inayowasukuma Wazaramo kutumia tungo za kifutuhi wakati wa kuimba nyimbo za sherehe za unyago. Sehemu ya pili inazichambua tungo za kifutuhi zilizopo katika nyimbo hizo na kuzitolea ufafanuzi, kulingana na maelezo yaliyopatikana kutoka kwa watafitiwa. Sehemu ya tatu inahitimisha kwa kujadili dhima mbalimbali za tungo za kifutuhi zilizopo katika nyimbo hizo. Katika kila sehemu ya sura hii, data zilizokusanywa kulingana na kila swali la utafiti huu zimefafanuliwa kwa njia ya maelezo kwa kuongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo msingi wake mkuu ni kuzitazama kazi za kifasihi kama akisio la maisha halisi ya watu.

## 4.2 Miktadha Inayozungukia Nyimbo za Sherehe za Unyago wa Wazaramo

Matumizi ya tungo za kifutuhi katika nyimbo za unyago wa Wazaramo hayatokani na hisia ombwe za watunzi au waimbaji. Aidha, ipo miktadha mbalimbali ndani ya tukio hilo ambayo hutoa msukumo wa kutumika kwa tungo hizo ili kubeba dhamira lengwa za nyimbo hizo kwa hadhira. Kabla ya kuifafanua kwa kina miktadha hiyo, ni vema kuanza kwa kutoa ufafanuzi mfupi kuhusu muundo na utendekaji wa nyimbo wakati wa sherehe za unyago wa Wazaramo.

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni mwa tasnifu hii, Wazaramo wamekuwa na utamaduni wa kuimba nyimbo mbalimbali katika sherehe za unyago ambazo hufanyika katika nyakati tofauti. Nyimbo hizi huzingatia ufundi mkubwa katika uimbaji ili kuweza kufikisha ujumbe wake kwa urahisi na kwa kuzingatia ubunifu mkubwa. Kimuundo, nyimbo hizi zimejipambanua vema katika vipengele vya fani, hususani vina na mizani, na kuzifanya ziweze kukaririka, kuimbika na kueleweka vema kwa hadhira yake. Urari huo wa vina na mizani katika uimbaji huenda sambamba na mrindimo wa ngoma, manyanga na debe ambavyo hupigwa kwa pamoja kiufundi na kuleta furaha miongoni mwa Wazaramo. Kwa kawaida, uimbaji na utendekaji wa nyimbo hizi huhusisha pande mbili, mwimbaji au mwanzilishi pamoja na waitikiaji. Imezoeleka kuona kuwa, nyimbo nyingi za shughuli za kijamii huwa ni mali ya jamii nzima. Mmiliki wake huwa hajipambanui wazi na hivyo kumfanya kila mmoja kuwa na uhuru wa kuziimba. Utafiti umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa nyimbo ziimbwazo wakati wa sherehe za unyago wa Wazaramo kwa sasa zimekuwa ni mali ya mtunzi. Yeye ndiye mwenye uhuru wa kuamua wimbo wake uimbwe wakati gani, na umdhamirie nani katika sherehe hiyo. Hivyo, kila wimbo uimbwao katika sherehe hizi, huwa na lengo maalumu ambalo mwimbaji amedhamiria kulifikisha kwa hadhira iliyomzunguka, ambayo yaweza kuwa ni majirani, ndugu, marafiki, au mwali anayefanyiwa sherehe. Hapo ndipo sanaa ya ufinyangaji wa lugha, ikiwepo utumizi wa tungo za kifutuhi, hutumiwa ili kubeba dhamira za waimbaji ambazo, kwa kiasi kikubwa hushabihiana na matukio halisi yanayowatokea. Ni katika miktadha ifuatayo ambapo watunzi na waimbaji hulazimika kutumia tungo mbalimbali za kifutuhi wakati wa sherehe za unyago wa Wazaramo:

### 4.2.1 Utani

Matumizi ya tungo za kifutuhi wakati mwingine husukumwa na hisia za utani walizonazo watunzi na waimbaji wa nyimbo za unyagoni. Sengo (1975) anafafanua dhana ya utani kuwa ni neno la kiswahili lihusulo mwenendo au utaratibu wa maisha unaoingiliana na mila na desturi kadha wa kadha katika jumuia za wenyeji wa Afrika ya Mashariki. Anazidi kufafanua kuwa utani katika jamii za Kiafrika ni zaidi ya mzaha. Tangu zamani utani ulitumika kuwapatanisha wanyonge na wenye nguvu kwa kuandaa mbinu ya mawasiliano. Hali kadhalika, suala la utani kwa Wazaramo ni la kawaida, na limekuwa ni sehemu ya mfumo wa maisha ambao umezoeleka na kila mtu. Huu, waweza kuwa kati ya mtu na mtu, familia kwa familia, ukoo kwa ukoo, au Uzaramo dhidi ya jamii nyingine, ilimradi pande zote ziufahamu na kuuridhia mfumo huu wa kimaisha. Msingi mkuu wa utani katika jamii yoyote hapa Tanzania, ni mawazo ambayo hutokana na ukweli. Hivyo, dhana ya utani hutumiwa ili kufikisha mawazo yaliyo mazito ambayo humhusu mtu au kundi la watu; na mawazo hayo aghalabu huwa ni ya ukweli mtupu ijapokuwa huwasilishwa mbele ya hadhira kwa kigezo cha utani.

Utani huwafanya Wazaramo kuwa huru kutamka na kutenda mambo mbalimbali wakati wa sherehe za unyago; na hivyo, kuwafanya pia watumie tungo za kifutuhi kama vile kejeli, vijembe, balagha, na dhihaka ambazo zote hutawaliwa na hali ya ucheshi, na kuibua fikra ili kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

### 4.2.2 Haja ya Kuwafumbia Mahasimu

Hisia za hofu na wasiwasi wakati mwingine huwasukuma Wazaramo kubuni na kutumia mbinu za kifutuhi ili kuweka wazi mawazo yao ambayo aghalabu huwa ni ya kero. Sherehe za unyago katika jamii ya Wazaramo huwakutanisha watu wengi

toka maeneo mbalimbali ambao baadhi yao; miongoni mwao wapo wenye chuki na uhasama wa muda mrefu. Hali hiyo husababisha pande hizo mbili kutumia uwanja huo ili kusutana, kung'ong'ana, na kuambiana ukweli kwa njia ya uimbaji, kutokana na matukio yaliyotokea awali yakiwahusu wao. Matukio yanayojitokeza zaidi ni yale yanayohusiana na mfumo wa maisha na namna jamii inavyoishi; kwa mfano umbea, kuchukuliana waume au wake, ubinafsi, tamaa, choyo, na uvivu. Wakati mwingine hofu ya kutokea kwa vurugu za ana kwa ana hutokea, hususani migogoro hiyo inapofafanuliwa kwa uwazi kwa kutaja jina halisi la mtu aliyehusika, sifa zake, au tukio analohusishwa nalo. Hapa ndipo sanaa ya ufutuhi hutumiwa na watunzi ili kupunguza ukali wa mabishano hayo. Kwa mfano, baadhi ya nyimbo zilizoshughulikiwa katika utafiti huu, zimetaja majina ya watu kisanaa, kwa lengo la kuwianisha sifa zao, na sifa za walengwa wa dhamira za wimbo husika.

### 4.2.3 Kuendeleza Historia

Huu ni msukumo ambao chimbuko lake hasa ni mfumo wa maisha ambao ulitumiwa na Wazaramo tangu zamani na kuigwa na hawa wa sasa. Kutokana na ufafanuzi uliopatikana kutoka kwa baadhi ya watafitiwa, imebainika kuwa matumizi ya kejeli, vijembe, dhihaka, na balagha hayakuanza sasa. Jamii imekuwa ikirithi na kufuata mitindo mbalimbali ya uimbaji iliyoasisiwa na wazee wa Kizaramo ambao waliishi miaka iliyopita. Hata hivi sasa, wapo baadhi ya Wazaramo ambao huona sherehe za unyago kuwa ni sehemu ya kupeana ukweli kwa njia za kifutuhi kama walivyofanya waliotangulia. Hivyo, jambo hili limekuwa ni chachu ya kuwafanya waendelee kutumia sanaa hii ya uimbaji ili kubeba dhamira zao kila yafanyikapo matukio ya sherehe za unyago yanayowahusu watu wa jamii hii.

### 4.2.4 Kuendeleza Usemezano

Katika tasnifu hii dhana ya Usemezano inachukuliwa kuwa ni hali ya kuelezana ujumbe kwa namna ya kubadilishana. Suala hili huweza kufanywa baina ya watu wawili au zaidi. Zaidi, huweza kudumu hata kwa miaka kadhaa (watu wakiendelea kujibizana mambo mbalimbali kupitia matukio kama la sherehe za jando ambalo limezamiwa na utafiti ulifanywa). Mjadala huu endelevu hufanywa na Wazaramo ili kufafanua na kuelezana mambo mbalimbali yanayowahusu. Usemezano katika jamii hii ni suala la kawaida kwa sababu huwafanya wahusika kuwa huru kuyasema yale wanayoyafikiria kuhusu mtu au kundi lingine hasimu. Vitendo hivi huanzia katika mazingira na maisha ya kawaida ya wanajamii. Wakati wa sherehe za unyago, watu huwa huru zaidi kwa sababu ni tukio ambalo huwafanya watu kucheza na kuimba kwa furaha. Hapa ndipo Wazaramo wengi hukutana huku kila mmoja akiwa na jambo lake ambalo hudhamiria kuliweka hadharani. Watunzi na waimbaji wa nyimbo za sherehe, huamua kutumia tungo zenye vijembe, kejeli, dhihaka na balagha ili kuweka wazi mawazo yao.

Kauli za kifutuhi katika muktadha huu ambazo aghalabu huwalenga watu mahsusi, husababisha kuibuka kwa hisia na haja ya baadhi ya watu kulipa kisasi. Hili hutokea pale watu hao wanapoguswa na maudhui yaliyopo katika tungo zake. Katika muktadha wa kisherehe, visasi vinavyozungumziwa hapa si vile vinavyowakutanisha mahasimu katika malumbano ya kutumia nguvu au silaha. Tungo za kifutuhi kama hizo zinazolenga kujibu mashambulizi hayo, ndizo huwa na nafasi kubwa katika kuoneshana uhodari wa kusemezana kati ya pande mbili.

### 4.3 Tungo za Kifutuhi Zinazojitokeza katika Nyimbo za Unyago wa Wazaramo

Kutokana na ufafanuzi wa hapo juu uliohusu miktadha mbalimbali inayowasukuma Wazaramo kutumia tungo za kifutuhi, ufuatao ni mjadala kuhusu jinsi nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo zinavyojumuisha tungo za hizo. Mjadala huu kwa jumla unabainisha nyimbo ya unyago iliyoimbwa, maelezo ya jumla ya nyimbo hiyo, tungo za kifutuhi na maana zake kulingana na muktadha wa sherehe, pamoja na uhusiano wa nyimbo hiyo na uhalisi wake katika maisha ya kawaida ya jamii.

a) Wimbo wa Kwanza:

Wananiambia malaya, ninalalwa mihogoni x2
Hao watoto wa shekhe, sigida hatuzioni,

*Kiitikio*:
Ndugu zangu eee, wananiheleleza, najaribu najaribu kama nitaweza...

Wimbo huu ni wa sherehe za unyago, umebuniwa katika misingi ya kifutuhi kutokana na mkinzano wa kifikra baina ya pande mbili ambazo huibua ucheshi na kuleta fikra nzito kwa hadhira. Katika hali ya kawaida, malaya ni mtu mwenye tabia ya kupenda kufanya mapenzi na watu zaidi ya mmoja. Aidha, malaya hukosa subira katika kufanya uteuzi sahihi juu ya mtu, muda, na mazingira ya kufanyia tendo hilo. Kulalwa mihogoni ni hali ya kufanya mapenzi katika eneo la shamba lililopandwa mihogo. Kitendo hicho si cha kawaida kwa sababu mahali hapo si sahihi kwa kufanyia tendo hilo, na ni vigumu kwa mtu mwenye busara kufanya hivyo katika mazingira hayo. Aidha, shekhe ni kielelezo cha watu wafanyao matendo mema yanayopaswa kuigwa na wengine. Sigida ni alama nyeusi (mchubuko) katika paji la uso wa mtu inayotokana na msuguano wa muda mrefu kati ya ngozi ya paji la uso na mkeka ama jamvi la kuswalia. Katika jamii ya Wazaramo na jamii nyingi za hapa

Tanzania, alama hii huonekana kama ni kielelezo cha mtu afanyaye ibada hiyo kwa muda mrefu.

Katika wimbo huu, sanaa ya uburudishaji imetumika katika tungo zake ili kuleta akisio la maisha ya kawaida ya Wazaramo. Hali ya kutoonekana kwa sigida katika mapaji ya watoto wa shekhe imetafsiriwa kama kijembe kinachoashiria kuwa, pande zote mbili zinajihusisha na matendo yaliyo sawa. Kijembe hicho kinachokonoa na kung'ong'a sababu za maneno kuhusu tuhuma za matendo maovu yatokeayo ndani ya jamii nyingi kuelekezwa kwa upande mmoja tu. Hapa, ufutuhi unajitokeza kwa kuzihusisha pande mbili za wahusika zenye kukinzana kitabia. Kwanza, hali ya ucheshi kwa hadhira inaweza kujitokeza kwa kuvuta hisia za kujamiiana hususani katika shamba la mihogo. Ucheshi na fikra za watu zinaweza kuibuliwa zaidi na kitendo cha mtunzi kujielezea kwa kulinganisha tabia anazosemwa kuwa anazo, na tabia za watu wengine ambao kwa kejeli amewataja kama watoto wa shekhe.

Kwa kuzingatia mkondo unaoutazama uhalisia kama mbinu ya kisanaa, inaaminika kuwa sanaa iliyotumika katika kutunga wimbo huu haikutokana na hisia ombwe. Hii ni kwa sababu kuna uwiano mkubwa kati ya maudhui ya wimbo na hali halisi ya maisha ya watu. Ni wazi kuwa, vitendo vya baadhi ya wanajamii kujamiiana katika mazingira ya vichaka au mashamba vipo, hususani muda wa usiku wakati sherehe za unyago zikiendelea. Pia, kumekuwepo na wanajamii wengi ambao hufanya mambo kama hayo au yanayofanana na hayo kwa siri kubwa, na hivyo, kujulikana na watu wachache sana ndani ya jamii.

b) Wimbo wa Pili:

Mashehe wa Mkuranga, wamesoma kitabu gani? x2
Eti kumfukuza paka, mbwa kumuweka ndani,

*Kiitikio*:
Sema sema, sema sawasawa, usisahau kopo ukachambia upawa.

Miongoni mwa mambo ambayo hujitokeza na kushuhudiwa ni kuendelea kufanyika kwa matendo maovu kwa kujificha kupitia asasi za dini. Wazaramo wamekuwa na kawaida ya kuyakemea na kuyafichua mambo hayo wakati wa sherehe za unyago ambazo huwakutanisha watu wa kada mbalimbali kwa wakati mmoja. Kutokana na mfumo wa kimaisha ambao jamii imejiwekea, ni vigumu kuyakosoa maovu hayo kwa njia ya wazi kwani, kwa kufanya hivyo kunaweza kuibua migogoro au chuki kwa watu. Ndiyo sababu wimbo huu umejiegemeza katika misingi ya dhihaka na kejeli zenye kubeba maudhui hayo mazito kwa njia ya kisanaa. Kwa mfano ni katika mstari wa pili, ambapo tunakutana na tungo ya kifutuhi isemayo "eti kumfukuza paka, mbwa kumuweka ndani". Ufutuhi huu umebuniwa katika misingi ya kejeli ambayo imejengwa na unyume uliopo katika jambo hilo.

Kwa imani za dini ya Kiislamu, paka ni myama wa kawaida ambaye hana kipingamizi kwa Mwislamu yeyote kumfuga, lakini si jambo la halali kwao kufuga mbwa. Wimbo huu pia umetumia lugha ya kijembe kwa kuwataja mashekhe kuwa wanafanya mambo kinyume, kwa kufuga mbwa badala ya paka. Hili ni jambo ambalo linaweza kuibua ucheshi na fikra kwa msikilizaji, pindi avutapo hisia za uhalisia wa jambo hilo. Aidha, mashekhe wametajwa katika wimbo huu kisanaa ili kuweka mshindilio wa wazo la mtunzi, ili kukwepa kuzua malumbano na waumini wa dini hiyo. Kiitikio cha wimbo huu kimebeba dhana ya balagha, ambayo pia, msingi wake mkuu ni kuwa na tungo zenye kuibua ucheshi mwingi. Hapa pia

tunabaini ufutuhi mwingine kwa kuwa katika msingi wa kihalisia ndani ya jamii, watu wengi hutenda mambo ambayo huenda kinyume na maadili ya jamii zao; yaani kuacha kufanya mambo mazuri na kuamua kufanya mambo yasiyofaa ambayo katika wimbo huu yamelinganishwa na kitendo cha kuchambia upawa badala ya kopo. Kwa maoni ya mtafiti, lengo kuu la wimbo huu ni kuwapasha wale wote wenye tabia ya kufanya maovu mengi ya chinichini huku wakijifanya wao kuwa ni washika dini. Watu hawa wamekuwepo kwa muda mrefu, wapo, na wanaendelea kuongezeka ndani ya jamii nyingi za Kitanzania.

c) Wimbo wa Tatu:

Mwanangu Ashura uwajue ndugu zako, x2
Usiwe dhaifu kama mimi mama yako,
Ninachukua watoto ninakwenda kuwatesa,
Hata shule ya msingi nashindwa kuwasomesha

Suala linaloibuliwa katika wimbo huu ni kuhusu malezi kwa watoto. Dhamira yake hasa ni kutoa dukuduku kwa njia ya vijembe kuhusu malezi ya watoto. Malezi kwa watoto katika jamii ya Wazaramo ni suala linalohusisha wanajamii wote. Ni jambo la kawaida kukuta watoto wakilelewa na ndugu wa pembeni ambaye si mzazi wake halisi. Tafsiri kuhusu ubora wa malezi apewayo mtoto hutofautiana kati ya mtu mmoja na mwingine. Wapo baadhi ya watu huona kuwa ndugu wa pembeni huchangia katika kutoa malezi mabaya kwa watoto kutokana na imani kuwa, wao hawana uchungu na watoto ambao si wao. Hivyo, huwanyanyasa au kuwatesa. Pia, wapo ambao huona kuwa malezi ni malezi tu; kwamba, malezi yatolewayo ni ya kawaida isipokuwa kinachowasumbua watu ni fikra ambazo zimeshazoeleka kuwa siku zote mzazi wa pembeni hawezi kutoa malezi mazuri kwa mtoto asiye wa kwake.

Baadhi ya nyimbo za unyago wa Wazaramo huakisi uhalisi; na wakati mwingine huwa ni simulizi za matukio yaliyowahi kutokea. Mfano mzuri ni wimbo huu. Mtunzi wa wimbo huu ni Mama Rahma, ambaye ni mhanga wa tukio hilo la malezi. Yeye ndiye aliyebeba jukumu la kumlea mtoto anayetajwa wimboni tangu akiwa mdogo mpaka kufikia hatua hiyo ya kuchezwa unyago.

Tungo za wimbo huu, hususani mstari wa pili hadi wa nne, zinatubainishia maneno ya kejeli ya mtunzi dhidi ya kundi fulani la watu. Hii ni kwa sababu maneno hayo ameyasema kama mwigo wa maneno ambayo ni kweli yalisemwa na watu wengine kuhusu yeye, juu ya mfumo wake wa kulea watoto wa ndugu zake. Hii inawiana na maoni ya Wamitila (2008) kwamba ili mtu aweze kuelewa kwa undani kuhusu tungo za kejeli zitolewazo na wanajamii na maana zake, hana budi kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu jamii husika ambayo tungo hizo hutumika. Hali ya ucheshi au tabasamu katika wimbo huu ilijitokeza pale hadhira iliposikia mwimbaji akiyasema kwa kejeli maneno ambayo hapo awali yalisemwa na watu wengine yakielekezwa kwake. Njia hii ya unyume wa kimatamshi, imetumiwa ili kutoa kero za mtunzi ambapo hadhira iliyokusanyika hususani maadui zake waliowahi kuyasema maneno hayo, ndio waliopata ujumbe huo zaidi ya watu wengine ambao hawajatamka.

d) Wimbo wa Nne:

Kinyago cha kimakonde kinaanza ujeuri x2
Mungu kakinyima sura, hata maneno mazuri,

*Kiitikio*:
Nilikuwa mbali, sasa nasogea karibu,
Namtaka mshambenga, aje nimtie aibu.

Huu ni wimbo wa sherehe za Wazaramo ambao umetawaliwa na lugha ya kitaswira inayoibua na kubeba maudhui mazito. Kimsingi, kinyago ni sanamu inayotengenezwa kwa kutumia mti, udongo au plastiki. Aghalabu, kinyago huwa na

sura ya kuchekesha na wakati mwingine sura ya kutisha. Tungo za wimbo huu zinaleteleza kuwepo kwa ufutuhi kutokana na kusheheni kwa dhihaka na balagha ndani yake, ambazo kwazo huibua hali ya ucheshi. Tungo isemayo "Mungu kakinyima sura", ni dhihaka kutokana na sababu mbili; kwanza, kinyago kina sura inayoonekana wazi. Pili, sura au mwonekano wa kinyago ni matokeo ya maamuzi ya kibunilizi yafanywayo na mwanadamu wakati wa kukiumba kinyago. Hivyo, kukihusisha na uumbaji wa Mungu pia, ni dhihaka. Kwa maoni ya mtafiti, hii inaashiria kiwango cha juu kabisa cha ubaya wa sura; ambapo, katika muktadha wa kifasihi, kinyago hicho kinaweza kuashiria mtu halisi na mahsusi, ambaye pia ndiyo mlengwa wa dhamira za wimbo huu.

Kwa upande mwingine, tungo "hata maneno mazuri", ni bunilizi ya kibalagha kwa kuwa kinyago si kiumbe hai. Kamwe hakiwezi kuwa na uwezo wa kutamka maneno ambayo yanaweza kutengwa katika makundi ya uzuri na ubaya. Hivyo, kukipa sifa ya ziada ya kutamka ni mbinu ya kisanaa katika uimbaji ili kurahisisha ubebaji wa maudhui ya wimbo. Dhihaka na balagha hizo ndizo zinazotusababishia ufutuhi ambao mtunzi amejaribu kuutumia ili kufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Kwa kuzingatia msingi wa nadharia ya uhalisia, wimbo huu unamhusu mtu au watu wenye tabia ya kusema maneno mengi ya umbea kuhusu watu wengine. Watu hawa wanathibitika katika jamii nyingi, na wamekuwa ni kero kwa wanajamii wengine. Ili kuonesha msisitizo kuhusu kuchoshwa na kundi hili, mwimbaji anajikweza mbele ya hadhira kwa kumtaka mtu mmojawapo mwenye sisa hizo ili amtie aibu.

e) Wimbo wa Tano:

Dada kanambia ngoma, bado siku tano x2
Leo siku imefika, ndugu yangu nitakupa nini?

*Kiitikio*:
Nakupa kologeti na mswaki, nataka roho yako iwe safi.

Suala linalojitokeza katika wimbo huu ni kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa za mwaliko wa sherehe za unyago. Wimbo huu ni mojawapo kati ya nyimbo nyingi zinazojaribu kutoa hisia za Wazaramo kuhusu jambo hilo. Kama ilivyoelezwa katika usuli wa tatizo la utafiti huu, maandalizi ya sherehe za unyago hufanywa kwa miezi kadhaa ili kutoa fursa kwa ndugu, jamaa, na marafiki kujiandaa kwa zawadi za wahusika wa sherehe hiyo. Taarifa za mwisho kwa wale ambao hawakuzipata mapema hutolewa siku ya Ijumaa ya wiki ya sherehe, kwa ngoma mahususi iitwayo mbiga ama kibiga, ambayo mbali na jukumu hilo, pia hutumiwa kama kiashiria cha kuanza rasmi kwa sherehe za unyago. Katika jamii ya Wazaramo, kitendo cha kutotoa au kucheleweshа taarifa za mwaliko kwa mtu hutafsiriwa kama dharau kwake na kutojali ama kutothamini mchango wake katika sherehe hiyo. Aidha, mhusika mkuu katika maandalizi ya sherehe hiyo maarufu kama mama shughuli au baba shughuli ndiyo hupewa lawama zote toka kwa watu hususani wale ambao hawakubahatika kupata taarifa hizo.

Tungo zilizotumiwa katika wimbo huu, kwanza, mwimbaji anaanza kwa kujiuliza kuwa atampa nini dada yake ikiwa hakupata muda wa kutosha kujiandaa kwa sherehe?. Kiitikio cha wimbo huu “nakupa kologeti na mswaki, nataka roho yako iwe safi”, kimetawaliwa na kaida za kifutuhi hasa kutokana na kujipambanua kwake katika misingi ya kukejeli. Ufutuhi huu hujitokeza zaidi pale hadhira inapohusisha moja kwa moja kiitikio hiki, na tabia halisi za huyo dada wa mtunzi ambazo zinafahamika na wanajamii. Kihalisia, kologeti, yaani ‘*colgate*’ na mswaki ni vitu ambavyo hutumika kwa ajili ya kusafisha meno. Kwa maoni ya mtafiti kuhusu

wimbo huu, lengo la mwimbaji si kumpa dada yake vitu hivyo kwa ajili ya matumizi ambayo yamezoeleka na kila mtu, bali amevitumia katika mwelekeo wa kukejeli ili kufikisha ujumbe wake. kuwa dada yake ana roho mbaya ambayo inahitaji kubadilika (Kusafishwa kwa kolgeti na mswaki).

f) Wimbo wa Sita:

Moza kanambia ngoma, mbele kuna siku kumi x2
Umenidharau kwa kuwa mimi muhuni,

*Kiitikio*:
Huniwezi dada huniwezi, mshahara wangu hauna mwisho
wa mwezi.

Miongoni mwa mambo ambayo Wazaramo huwa hawapendi kuonekana wameshindwa ni suala la kushiriki katika sherehe za unyago. Wakati mwingine, Wazaramo hujinyima au husitisha kufanya mambo mengine ya kiuchumi ili waweze kushiriki kikamilifu katika sherehe, na jamii iwatambue kuwa wameshiriki ipasavyo. Hali hiyo imesababisha Wazaramo watambulike kwa sifa kuu ya kuwa jamii inayopenda sherehe kuliko jamii nyingine za hapa Tanzania. Wengi huchukizwa na kutoshirikishwa kikamilifu katika maandalizi ya sherehe. Hivyo, watunzi hutumia sherehe hizo kutoa kero, mafundisho au madukuduku yao kuhusu kutoshirikishwa kama ilivyofafanuliwa katika wimbo wa tano. Pia, waimbaji wa nyimbo hizo hutumia uwanja huo na sanaa hiyo ya nyimbo ili kuthibitisha uhodari wao na utayari wao katika kushiriki tukio hilo kwa hali yoyote.

Katika wimbo huu, kiitikio chake kisemacho “huniwezi dada huniwezi, mshahara wangu hauna mwisho wa mwezi”, kimetawaliwa na majigambo na vijembe ambavyo kwa pamoja vinaubainisha ufutuhi uliopo katika wimbo huu. Katika maisha ya kawaida, imezoeleka kuona kuwa, watu wengi hususani watumishi hupata mishahara

yao kipindi cha kila mwisho wa mwezi. Hali hiyo pia, husababisha kuongezeka kwa mzunguko wa pesa hata kwa watu wengine ambao si watumishi, na hivyo kipindi cha mwisho wa mwezi kuonekana ni kipindi cha watu wengi kuwa na pesa. Wimbo huu unaibuka na mtazamo tofauti uliobebwa na kijembe kinachotupwa kwa muandaaji wa sherehe hiyo na hata watu wengine wanaotarajia kuandaa tukio kama hilo kuwa, mwimbaji yupo tayari kufanya jambo muda wowote kwa kuwa anao uwezo mzuri kiuchumi; na kwamba katu hategemei mshahara wa mwisho wa mwezi kama ilivyozoeleka kwa watu wengi.

g) Wimbo wa Saba:

Wewe dada Rukia unilelee wanangu,x2
Dada Mwanahawa ongeza nauli yangu,
Na wewe dada mkubwa unipeleke safari yangu,

*Kiitikio*:
Poleni ndugu zangu nawaachieni tabu,
Ninakwenda Loliondo kunywa kikombe cha babu.

Neno Loliondo linakumbushia tukio la kuibuka kwa tiba mbadala maarufu kama “kikombe cha babu”, iliyopata kutolewa na mchungaji Ambilikile Mwaisapila, maarufu kama Babu wa Loliondo. Umaarufu wa babu huyo ulikuja ghafla kutokana nguvu ya tiba yake (kikombe) kwa wale walioiamini ukilinganisha na bei yake ndogo ya shilingi mia tano. Hali hiyo ilisababisha watu mbalimbali wenye magonjwa tofauti toka ndani na hata nje ya nchi kufika kwa wingi eneo hilo ili kupata tiba hiyo. Iliaminika kwamba, kila aliyekwenda Loliondo alikuwa na magonjwa sugu yaliyoshindikana kutibika kwa njia nyingine na hivyo kuhitaji muujiza wa babu.

Wimbo huu umepambwa na kaida za kifutuhi kutokana na kuwepo kwa kijembe ambacho kinaleta ukinzani wa kimaana kati ya tungo zilizotumika na uhalisia wa tukio kulingana na ufafanuzi wake alioutoa. Huu ni wimbo wenye uhalisi. Utafiti

umebaini kuwa mtunzi wake aliwahi kupata matatizo ya kiafya katika nyakati fulani. Matatizo hayo yalimchukua muda mrefu kupona. Ni kawaida kwa wanajamii kuhisi matatizo yanayomsumbua mtu bila ya kupata ithibati ya kidaktari. Hivyo, wapo wanajamii waliomtangaza kuwa ni mwathirika wa UKIMWI. Lakini, baada ya juhudi za kimatibabu aliweza kupona kabisa. Hivyo, mistari mitatu ya kwanza ya wimbo huu imejengeka kifutuhi kwa kuwa inawataja dada zake na majukumu anayowaachia wakati wa safari hiyo. Majukumu hayo yana uhalisia kutokana na dada zake hao kuwa katika hali hizo katika maisha yao. Akifafanua kuhusu hilo, mtafitiwa ambaye pia ni mtunzi anasema:

> Fatuma ni dada yangu wa kwanza. Kutokana na hali yake ilivyo, yeye nimeamua kumuomba anisindikize katika safari yangu. Rukia nimemwambia anilelee wanangu kwa sababu yeye ana juhudi katika kulea watoto kwani hata mimi amenilea yeye na kunisomesha, na hata mwanangu Rahma mara nyingi anaishi kwake. Mwanahawa pia nimemuomba aniongezee nauli kwa sababu yeye Mungu amemjalia kuwa na kazi nzuri na kipato kizuri...[5]

Dondoo hili linaonesha mgawanyo wa majukumu anayoyatoa mwimbaji kwa ndugu zake kulingana na hali zao. Wimbo huu ulisababisha kuibuka kwa hali ya ucheshi hasa kwa hadhira ambayo inawafahamu ndugu hawa na maisha yao kwa ujumla hasa baada ya kusikia maisha hayo yameibukia katika nyimbo ya unyagoni.

Ni katika kiitikio cha wimbo huu, ambacho kinataja safari ya Loliondo kwa ajili ya kwenda kupata tiba ya kikombe cha babu, ndipo tunapopkutana na dhana ya ufutuhi. Hii ni kwa sababu tungo zote hizo zimetumika kurusha kijembe kwa wanajamii waliokuwa wakivumisha kuwa ni mwathirika wa UKIMWI. Aidha, katika uhalisia wake, mwimbaji alikuwa ni mzima wa afya wakati akiimba wimbo huu, na hapakuwa na dalili yoyote ya yeye kuzidiwa mpaka kuhitaji tiba hiyo ya kikombe.

[5] Mazungumzo kati ya mtafiti na Mama Rahma siku ya Jumapili tarehe 8/12/2013, katika kijiji cha Kibamba, wilayani Mkuranga.

h) Wimbo wa Nane:

Umelilia mkole, leo nakupa mwanangu, x2
Ukiniita mama, nami nitaitika bee mwanangu,
Ukiniona fungo, nami nakuona paka, unakunya jikoni kwangu

Wimbo huu umetungwa katika misingi ya mazungumzo kati ya mama na mtoto wake. Mazungumzo haya yanaonekana kujikita zaidi katika kutoa onyo kali kwa mtoto kuhusu kumtambua mama yake. Lugha teule ya mtunzi wa wimbo huu imetawaliwa na maneno makali ya dhihaka na kejeli ambazo, ndizo zibebazo maudhui ya wimbo mzima. Kwanza, mtunzi ametumia tungo "ukiniona fungo" kama mwangwi wa fikra ambazo mtoto wa kike anaweza kuwa nazo dhidi ya mama yake, hususani baada ya kuchezwa unyago. Kihalisia, fungo ni mnyama ambaye anafahamika kwa sifa yake ya kuwa mchafu, harufu mbaya, na rangi yake nyeusi tii. Hivyo, kitendo cha mtoto kumuona mama yake kama fungo ni namna ya kisanaa inayomaanisha vitendo vya dharau na kushushwa kwa thamani ya mama kunakojitokeza sana ndani ya jamii. Katika mstari huohuo, mtunzi anaposema "nami nakuona paka, unakunya jikoni kwangu", anaashiria majibu ya kejeli ambayo pia hutolewa na wazazi ambao huonekana kutojali tabia mbaya za watoto wao ambazo huibuka baada ya kufunzwa mambo ya utu uzima wakati wa unyago.

Kudhihirika kwa ufutuhi katika wimbo huu kunatokana na tungo hizo za mama na mtoto wake, ijapokuwa zote zimeimbwa na mtu mmoja. Hii inatokana na hadhira kuibua fikra zao kwa viumbe halisi waliotajwa wimboni na sifa zao. Kwa hakika fungo na binadamu ni viumbe wa haiba tofauti. Pia, kitendo cha kumlinganisha mtu na paka mwenye sifa za kujisaidia jikoni, si cha kawaida na hivyo kuwafanya watu watabasamu huku wakifikiria kwa kina kile kisemwacho na mtunzi.

Kwa ujumla, lengo la wimbo huu si kuchekesha hadhira kwa kulinganisha binadamu na viumbe wengine wasio binadamu, bali ni kukemea vikali tabia zote mbaya kwa watoto wa kike ambao wanaweza kuwa ni wahusika wa sherehe hiyo (wali), au wasichana wengine miongoni mwa hadhira iliyokusanyika.

i) Wimbo wa Tisa:

Maneno mliyosema, mwenyewe nimeyasikia, x2
Lakini mimi mwana mdogo, naweza kuvumilia,

*Kiitikio*:
Mama eee njoo nifuate,
Uniongeze mafundo nijue kukaa na wakwe.

Msingi mkuu wa kufanyika kwa sherehe za unyago wa Wazaramo ni kumfunza binti wa kizaramo namna ya kujitambua na kuishi vizuri na watu, hususani, wakati atakapoolewa. Miongoni mwa watu ambao msichana husisitizwa kuwaheshimu ni wakwe zake. Kwa upande mwingine, Wazaramo wanaamini baadhi ya wakwe huwa ni chanzo cha kuyumba kwa familia nyingi. Jambo hilo pia huwasukuma watunzi wa nyimbo za sherehe za unyago, kulizungumza kwa njia ya nyimbo zilizojaa tungo za kifutuhi ambazo hubeba dhamira mbalimbali dhidi ya vitendo hivyo.

Kwa mfano wimbo huu wa unyago umetawaliwa na viashira vya kifutuhi ambavyo kwavyo, huleteleza kuwepo kwa ucheshi kwa hadhira, huku ukiibua fikra nyingi kuhusu maudhui yake. Mstari wa kwanza wa wimbo huu ni kijenzi cha ufutuhi kinachojipambanua katika msingi wa dhihaka kwa kundi fulani la watu. Katika hali ya kawaida, walengwa wa hapa ni wale ambao kwa namna moja au nyingine, walitamka maneno fulani ambayo mwimbaji anadai kuwa tayari ameshayafahamu, na kwamba, hayapo tena katika hali fiche ya kuteta. Aidha, kiitikio cha wimbo huu ni kijembe cha wazi ambacho kinapigwa kwa wakwe. Kipande mstari cha mwisho katika kiitikio chake ni kijembe, ambapo ukiutazama wimbo huu kwa ujumla wake,

mwimbaji anawakilisha wanawake walio katika maisha ya ndoa, wamekomaa kifikra kutokana na mafundo yahusuyo unyago na jinsi ya kuishi na watu wa kada mbalimbali wakiwapo wakwe. Hivyo, maneno yote mabaya wayasemayo wakwe, ni matokeo ya chuki na udhaifu wao wenyewe.

j) Wimbo wa Kumi:

Walikuwa wanateta, visimani kwenye kuni, x2
Rehema ana mimba, mkole atamcheza nani?

*Kiitikio*:
Wako wapi washambenga tuwashike pua,
Waliosema hayawi, mbona leo yamekuwa.

Wimbo huu huimbwa katika mkusanyiko wa sherehe za unyago ukiwa na dhamira tofauti. Wazaramo huamini kuwa kitendo cha msichana kupata mimba kabla ya kuchezwa unyago au kabla ya kuolewa kuwa ni fedheha kwa familia ya binti hususani mama mzazi au mlezi. Hii ni kutokana na imani kwamba, unyago ni tukio adhimu ambalo msichana wa Kizaramo hupaswa kufundishwa mambo yote ya kiutu uzima likiwamo suala la uzazi na malezi.

Washambenga ni jina la kikejeli ambalo humaanisha kikundi cha watu hususani wanawake wenye kupenda kuzungumza mambo ambayo hayawahusu au wasiyokuwa na uhakika nayo. Hali hiyo inapojitokeza, wapo Wazaramo ambao huamua kutoa hisia za nafsi zao katika mkusanyiko wa watu kwa njia ya nyimbo za unyago, hususani, pindi inapodhihirika kuwa kile kilichokuwa kikidhaniwa kimekuwa si sahihi au kutokuwa na madhara yale yaliyotazamiwa na wengi kutokea. Kuhusu sababu za kuutunga wimbo huu, mtunzi alieleza:

> Rehema ni mtoto wangu wa kumzaa mwenyewe. Kuna wakati ulitokea uvumi kuwa eti mwanangu ana mimba. Mimi nikayasikia hayo maneno ya umbea, na nilijua tu watu wangesema sana kama ingekuwa kweli. Nikaamua

> kumpeleka hospitali ili kumpima na kwa bahati nzuri hakuwa na mimba wala nini. Wimbo huu nimewaimbia watu ambao nawajua fika kwa kuwa wao ndio huwa na midomo ya haraka haraka kuyasema yasiyowahusu. Sijamtaja mtu jina lakini wenyewe wameshaipata habari yao...[6]

Dondoo hili linaonesha namna wazazi wanavyokuwa na furaha pindi watoto wao wa kike wanaponusurika na tukio la kupata mimba katika umri mdogo, na kabla ya kuolewa. Hivyo, vijembe vilivyomo katika wimbo huu ni sehemu ya mbinu ya kuonesha furaha hiyo, huku akidhamiria kuwapiga kijembe watu ambao walihusika kusema maneno hayo, na kudhani kuwa mimba ni jambo la ajabu ambalo msichana aliyekumbwa na kadhia hiyo hastahili kufanyiwa sherehe ya unyago. Mstari wa kwanza katika kiitikio ndio unaobainisha ufutuhi uliotumiwa na mtunzi wa wimbo huu. Dhana ya "kushika pua", hutumiwa sana na Wazaramo kumaanisha kitendo cha kumsuta, kumsema mtu, na kumuonya kutokana na vitendo vyake vya umbea. Wahusika wakubwa wa tukio hili huwa ni wanawake. Kihalisia, kitendo hicho hupokelewa kwa shangwe kubwa na kukusanya umati mkubwa wa watu kila kinapotokea ndani ya jamii.

Kwa ujumla wimbo huu unafafanua kero wanazozipata watu ndani ya jamii, kutokana na vitendo vya baadhi yao kusema maneno mengi wasiyokuwa na uhakika nayo. Hivyo, huleta urahisi wa kueleweka pindi wahusika hao wanapokuwa ni sehemu ya hadhira. Hawa huwekwa katika hali fiche ili kuepuka migogoro ya moja kwa moja kati ya watu.

[6] Mazungumzo kati ya mtafiti na Bi Zubeda Mlawa siku ya Jumamosi tarehe 11/1/2014

k) Wimbo wa Kumi na Moja:

Watu wananambia malaya kutwa kucha minazini x2
Sijui nyie wenzangu mlioziba huko chini,

*Kiitikio*:
Leo ni leo asiye na mwana pole yake,
Ukijitia umbea, hapa lazima uufyate.

Wimbo huu unafafanua tabia binafsi za mtu. Umetumia maneno makali yaliyotawaliwa na kaida za kifutuhi zenye kubeba ujumbe mzito kwa hadhira. Ni wazi kuwa nyimbo zote za sherehe za unyago wa Wazaramo ni mwangwi wa matukio halisi yaliyotokea au yanayoendelea kutokea ndani ya jamii. Suala la umalaya ndilo wazo kuu ambalo linajitokeza na kujenga maudhui ya wimbo huu. Hili, limefafanuliwa kisanaa na mtunzi kwa kutumia tungo zenye kejeli na dhihaka ambazo zinaibua fikra nyingi zenye kuambatana na ucheshi kwa hadhira. Katika hali halisi ya maisha ya watu, malaya ni mtu mwenye tabia ya kupenda kufanya mapenzi na wanaume zaidi ya mmoja, na wakati mwingine hata kwa wakati mmoja. Tungo "kutwa kucha minazini" imetumika kibalagha ili kusisitiza wazo kuu la mwimbaji kuhusu kiasi gani mtu anajihusisha na kitendo hicho. Hapa ndipo ufutuhi unajitokeza waziwazi. Hii ni kwa sababu kitendo cha kukaa kutwa kucha katika eneo hilo, kwa ajili ya kutenda kitendo hicho ni kigumu. Hivyo, huwaacha watu wacheke na kufikiri sifa hiyo na tabia halisi za mhusika.

Pia, tungo isemayo "sijui nyie wenzangu, mlioziba huko chini", ni kijembe kikali kinachopigwa dhidi ya kundi fulani la watu. Kutokana na mfumo halisi wa maisha ya Wazaramo, utafiti umebaini kuwa kijembe kilichopo katika tungo hii kinawahusu baadhi ya watu ambao wamekuwa wakimwona mtunzi na mwimbaji wa wimbo huu kuwa na matendo yanayoashiria umalaya. Tungo hii imebeba dhamira mahususi ambayo mwimbaji ameiweka katika hali fiche. Pia, ndiyo inayoibua ufutuhi

mwingine katika wimbo huu unaofanya watu wafurahi kutokana na ukweli kuwa, ni vigumu kwa mtu wa kawaida kuziba sehemu hizo za mwili bila kuwepo kwa sababu za msingi za kitabibu. Aidha, inaibua hisia za ngono kutokana na kauli zilizotumika kuibua mjadala pendwa ndani ya jamii hii na jamii nyingi za Kitanzania.

Kwa ujumla, lengo la mtunzi ni kuieleza hadhira na mahasimu wake kuwa umalaya ni sifa tu ambayo mtu huitoa kwa mwingine kulingana na mtazamo wake. Lakini ukweli ni kwamba tendo hilo ni la kawaida na hufanywa na watu wengi wasio na matatizo ya kiafya.

l) Wimbo wa Kumi na Mbili:

Domo la upa, limeanza uchokozi, x2
Mume wako sikumwita, kaja kusomea kozi,

*Kiitikio*
Ukitaka kupigana, uje kwetu Mkokozi
Ukusanye na wapambe, peke yako huniwezi

Kama ilivyo katika jamii nyingine za Kitanzania, madhumuni makuu ya kufanyika kwa sherehe za unyago kwa mabinti ni kuwaandaa kuyaanza maisha mapya ya kiutu uzima. Mbali na kubeba dhima hiyo, Wazaramo pia hutumia sherehe hizo kama uwanja wa "kusutana" ama kuambiana ukweli. Kila mwenye jambo lake ambalo lilimkera katika kipindi fulani, hukaa nalo moyoni mpaka siku ya sherehe ya unyago ambapo hulitoa hadharani kwa kutumia sanaa ya nyimbo. Suala linaloibuka katika wimbo huu ni kuhusu vitendo vya kuchukuliana wanaume ambavyo hujitokeza katika jamii nyingi ikiwepo jamii ya Wazaramo ambapo utafiti huu umefanyika. Matukio kama hayo husemwa hadharani ijapokuwa wahusika wake hawatajwi waziwazi, hivyo kutoa nafasi kwa kila anayedhani anahusika kwa jambo hilo kuupata ujumbe wake. Tafsiri ya tungo "domo la upa" katika wimbo hu ni mdomo

mchafu. Aidha, uchafu unaozungumzwa sio ule wa kawaida, bali ni hali ya kusemasema maneno mengi na ya hovyohovyo pasipo kuwa na uhakika nayo.

Katika wimbo huu, tungo isemayo “mume wako sikumwita, kaja kusomea kozi”, ni kijembe ambacho mwimbaji anakusudia kukifikisha kwa mwanamke ambaye mume wake anatajwa kufanya mapenzi nje ya ndoa. Tungo hii imekaa katika mtindo wa majigambo ambayo ndiyo msingi wa kuibuka kwa ufutuhi wa wimbo huu. Inafahamika kuwa kozi ni mafunzo maalumu ambayo hutolewa katika vyuo au taasisi kwa ajili ya kuibua ujuzi fulani. Hivyo, kitendo cha mtunzi kujilinganisha na chuo au taasisi ya mafunzo, hususani ya mapenzi kinazua ucheshi. Kwa maoni ya mtafiti, inaonesha kuwa lengo la mtunzi ni kuidhihirishia hadhira kuwa yeye ana uwezo mkubwa wa kumtunza mwanaume kuliko mwanamke anayempiga kijembe katika wimbo huu. Pia, kiitikio cha wimbo huu kimejengwa na bunilizi za kidhihaka ambapo mwimbaji anajaribu kujitweza mbele ya hadhira kuwa yeye si mtu wa kuumiza kichwa kuhusu suala hilo. Pia, ametaja kijiji halisi cha Mkokozi ambacho kipo jirani na kijiji cha Kibamba ambapo sherehe hii ilikuwa ikifanyika. Hili husaidia kujenga tabasamu, usikivu, na uelewa mzuri kutokana na kutumia kisanaa mifano halisi ijulikanayo na wanajamii. Mstari wa mwisho wa wimbo huu usemao “Ukusanye na wapambe, peke yako huniwezi” ni kijembe ambacho kinaweza kuchochea hamaki kwa upande wa pili unaotajwa katika tungo hizi. Hiki huzua taharuki kwa sababu ya ufundi wa kujitweza alioutumia mwimbaji kujionesha kuwa na uwezo wa ziada wa kukabiliana na watu wengi ambao watahitaji kuanzisha vurugu na mapigano dhidi yake kwa wakati mmoja.

Kwa ujumla, ufutuhi uliotumika katika wimbo huu unahalisika kwa kuwa ndoa ni hatua mojawapo ya kimaisha ndani ya jamii. Mbali na kuwepo kwa faida nyingi katika jambo hili, bado kumekuwepo na changamoto za kuoneana wivu kati ya watu na hata kufikia hatua ya kuchukuliana waume au wake kwa njia yoyote ili kufanya nao mapenzi. Tukio la sherehe za unyago katika jamii ya Wazaramo limeonekana kuwa ndilo muafaka kwao ili kulisemea na kulikemea kama ilivyofanyika katika wimbo huu.

m) Wimbo wa Kumi na Tatu:

Barazani kwangu nimeupanda mgomegome, x2
Ukitaka kuuchimba, ukae chini usome,
Wanaume wa wenzio, kuwachukua ukome,

*Kiitikio*:
Fungua dirisha, mpenzi naona joto,
Punguza mapenzi, na wewe bado mtoto

Malumbano na hali ya kujibizana maneno katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo hayaishii kwa kauli za upande mmoja tu. Wakati mwingine, kauli za kumtaka mtu kujibu maudhui ya wimbo fulani ambao umemgusa husikika kwa shangwe kubwa toka kwa hadhira iliyokusanyika. Hali hiyo husababisha kutokea kwa baadhi ya watu ambao huamua kuimba nyimbo tofauti ambazo hujibu zile zilizotangulia. Wimbo huu ni ithibati ya majibizano ya pande hizo; ambapo unajaribu kujibu kauli za kifutuhi zilizopo katika wimbo wa kumi na moja. Baadhi ya waimbaji huamua kuimba nyimbo za majibu ili kuwafurahisha watu tu, lakini siyo kila anayefanya hivyo basi anahusika kweli na mambo hayo. Mstari wa kwanza wa wimbo huu unadhihirisha kijembe kinachopigwa kwa mlengwa aliyewekwa katika hali kapa, ili kubeba dhamira ya mwimbaji.

Mgomegome ni mti mkubwa na mgumu upatikanao katika ukanda wa pwani. Sifa kuu ya mti huu ni kuwa na mizizi mirefu ambayo hujikita aridhini na kuufanya uwe imara. Katika wimbo huu, mti huu umetumika kitaswira kuashiria hali ya kujiamini kwa mtu kutoweza kutetereka katika ndoa yake. Mstari wa pili umejengeka kibalagha; ambapo, mwimbaji ametia chumvi ili kuzidi kuupa sifa za ziada mti huo. Suala la kusoma kabla ya kuuchimba limetumika kisanaa kuashiria kitendo cha mtu kujipanga na kujitosheleza kimbinu. Balagha hii ndiyo huibua ufutuhi kwa sababu inataja suala la kusoma na kulifanya kuwa ndio suluhisho la kuuchimba mti ambao, kwa maoni ya mtafiti umetajwa kisanaa tu. Ufutuhi katika wimbo huu, unajipambanua pia kwa kijembe cha wazi katika mstari wa tatu usemao "wanaume wa wenzio, kuwachukua ukome". Hali ya ucheshi katika tungo hii inatokana na hisia za kuwepo kwa usemezano wa wazi kati ya watunzi wawili katika sherehe moja. Hii ni kwa sababu, tungo hii inajibu waziwazi kijembe kikali kilichopigwa katika mstari wa pili wa wimbo wa kumi na moja kinachosema; 'mume wako sikumwita, kaja kusomea kozi'. Hivyo, dhamira kuu ya mtunzi ni kujibu, na kutoa onyo kali dhidi ya watu wenye tabia za kutembea waume za watu.

n) Wimbo wa Kumi na Nne:

Pili umetaka mkole, na mkole ndio huo, x2
Usigeuke malaya ukatembea na funguo,

*Kiitikio*:
Ukiitwa jifanye mnyonge kujikunyata,
Ukitaka mimba ya utoto utaipata.

Wakati mwingine waimbaji wa nyimbo za unyago wa Wazaramo hutumia tungo za kifutuhi zinazomlenga binti anayefanyiwa sherehe hiyo ya unyago (mwali). Baadhi ya mafunzo kwa mabinti hao hutolewa kwa siri kubwa na kushuhudiwa na kina mama watu wazima na wasichana ambao wameshachezwa unyago. Pia, yapo

mafunzo ambayo hutolewa hadharani kwenye mkusanyiko wa watu kwa njia ya nyimbo za sherehe au mazungumzo ya kawaida. Mstari wa pili wa wimbo usemao “usigeuke malaya, ukatembea na funguo” ni kijembe kwa msichana halisi; Pili. Kijembe hiki kinatoa taswira kuhusu tabia tarajiwa ambayo inaweza ikaanza baada ya kupata mafunzo ya utu uzima, kama ambavyo huwa inajitokeza kwa baadhi ya wasichana wanaobahatika kupata mafunzo hayo. Fikra kuhusu kazi halisi za funguo; yaani, kufungua kila inapohitajika kuingia ndani ndizo zinazoibua ufutuhi katika wimbo huu. Inahusishwa moja kwa moja na fumbo linalomaanisha mtu mwenye tabia ya kutojiheshimu na kuziachia sehemu zake za siri mara kwa mara kwa ajili ya kufanya mapenzi na watu mbalimbali. Kimsingi, utafiti umebaini kuwa si kila mafunzo ya unyago huleta matokeo mazuri ya kitabia kwa binti wa Kizaramo, kulingana na malengo na matarajio ya wana jamii. Baadhi ya mabinti hubadilika kutoka katika tabia nzuri kabla ya kubalehe na kuchezwa unyago, kwenda katika tabia mbaya baada ya tukio la sherehe hizo.

Katika mstari wa mwisho wa kiitikio, ufutuhi unajitokeza katika kijembe kingine kipigwacho moja kwa moja kwa binti huyo kuhusu matokeo ya tabia za umalaya ambazo anaaswa kutokuwa nazo. Kauli iliyotumika inaibua ucheshi kwa hadhira kwa kuwa imebuniwa katika misingi ya unyume. Hii ni kwa sababu mtunzi ametumia tungo hiyo kana kwamba maamuzi yote amemwachia msichana huyo. Lakini, kihalisia anakerwa na hapendi kuona jambo hilo likitokea. Aidha, zimetajwa mimba za utoto kwa kuwa ndizo zenye kuleta fedheha nyingi kwa familia za Kizaramo na hata hofu ya kutokea kwa madhara mbalimbali ya kiafya kwa msichana.

o) Wimbo wa Kumi na Tano:

Mama Zamda njoo nikupe maneno yako x2
Nimemkomoa mama Hamisi dada yako

*Kiitikio*:
Ulivyotoka huko dada mwenzio sikukujua
Guu moja funza, guu moja misusua.

Huu ni wimbo wa unyago ambao umetungwa kisanaa ili kufikisha mawazo mahsusi ya mtunzi kwa hadhira yake. Umejengwa na tungo zenye mwelekeo wa kifutuhi ili kubeba dhima lengwa kwa njia ya ucheshi. Majina yaliyotajwa katika wimbo huu ni ya wahusika halisi wanaofahamika vema na wanajamii wengine; na hivyo, kuakisi uhalisia wa maudhui ya wimbo huu. Uamuzi wa kutumia majina haya umetokana na sifa za wahusika hao na umaarufu walio nao katika eneo hilo; na hivyo, kuleta hali ya ucheshi kwa hadhira iliyokuwepo. Tungo zilizotumika katika kiitikio cha wimbo huu zina kejeli na dhihaka ambavyo kwa pamoja vinajaribu kutoa sifa zinazompambanua mlengwa. Mstari wa kwanza wa kiitikio chake usemao "ulivyotoka huko, dada mwenzio sikukujua", ni kejeli ambayo inakwenda sambamba na dhihaka isemayo guu moja funza, guu moja misusua". Funza na misusua ni magonjwa ya ngozi ambayo humpata mwanadamu. Aghalabu, magonjwa haya husababishwa na uchafu wa mazingira pamoja na uchafu wa mtu binafsi ikiwa ni pamoja na kutovaa viatu. Ufutuhi katika tungo hizi unajitokeza kutokana na taswira inayoibuka kuhusu mtu mwenye magonjwa hayo kwa wakati mmoja, na mhusika halisi ambaye katika muktadha huu amewekwa katika hali fiche, ijapokuwa mtunzi amemtaja mhusika wa kisanaa.

Kwa jumla, tungo hizi za kifutuhi zinalenga kuwafikia watu wote ambao hupokea mabadiliko ya kitabia hususani pindi wanapopata umaarufu au kuzoea mazingira. Awali, watu hawa huwa na hali mbaya, kama vile uchafu na uelewa hafifu wa

mambo. Lakini baadaye, watu hao hubadilika na kujiingiza katika tabia nyingine za ajabu kama vile ujeuri, ukosefu wa nidhamu kwa watu, ambapo huwa ni kero kwa jamii iliyowazunguka. Hivyo, tabia kama hizo huwa ni ajenda mojawapo inayotawala katika nyimbo za unyagoni ambapo huwa ni funzo kwa hadhira iliyokusanyika kushuhudia ama kushiriki katika sherehe hizo za kitamaduni.

p) Wimbo wa Kumi na Sita:

Nataka kusaula, mwenzenu najifikiria, x2
Matako sina, miguu imenikaukia,

*Kiitikio*:
Saula hivyo hivyo, kama ulivyozaliwa,
Usiogope wapambe, kwenda kukusimulia.

Wimbo huu wa unyago umebuniwa kwa kutumia maneno makali yenye kutoa wazo ambalo katika hali ya kawaida ni vigumu kutekelezeka isipokuwa katika muktadha wa kisherehe tu. Dhana za "kusaula", yaani kuvua nguo, na kauli kuwa "matako sina" ndizo zinazobeba wazo la msingi la mtunzi wa wimbo huu. Suala linaloibuliwa katika wimbo huu ni ithibati ya tabia walizonazo Wazaramo za kuwasema watu kuhusu maumbile yao ya mwili. Zaidi, wimbo umetuonesha namna Wazaramo wanavyoweza kutumia sanaa ya nyimbo, na muktadha wa unyago ili kulisawiri jambo hilo kwa undani. Katika wimbo huu, kunatajwa viungo kama matako, na miguu huku akidhamiria kulichopeka wazo lake analotaka kulifikisha kwa hadhira katika tungo hizo.

Tungo "matako sina" imetumika kama dhihaka na pia ni balagha; kwani, inatoa wazo ambalo kwa mtazamo wa nje linakwenda mbali zaidi ya uhalisia wa mambo. Kimsingi, watu wote huzaliwa wakiwa na viungo hivyo, isipokuwa kwa wale wachache sana ambao huwa na matatizo ya kimaumbile wakati wa kuzaliwa kwao. Pia, tungo "miguu imenikaukia" nayo ni dhihaka ya kimaumbile, ambapo, kukauka

kwa miguu kunajaribu kutoa taswira ama mwonekano wa miguu ambayo hutajwa kuwa ni midogo (myembamba). Ufutuhi katika wimbo huu unatokana na uwezekano wa watu kuelekeza fikra zao katika viungo hivyo vya mwili. Maumbile kama ‘matako’ yamekuwa ni kichocheo kikubwa cha ngono hususani yanapokuwa na ukubwa usio wa kawaida. Hivyo, kutajwa kwake huweza kuibua hali ya tabasamu miongoni mwa hadhira iliyokusanyika.

Katika muktadha wa kisherehe, imebainika kuwa hoja kuu ya wimbo huu ni kutoa ujumbe wa faraja kwa watu ambao wamekuwa wakiandamwa na wanajamii wengine kwa maneno ya chinichini yenye dharau kwa kuwa na maumbile yasiyo na mvuto machoni kwa watu. Hivyo, msuko wa tungo hizi umekaa kifutuhi ili kurahisisha kutoa wazo hilo kwa hadhira iliyokuwepo wakati wa kufanyika kwa sherehe hizo.

q) Wimbo wa Kumi na Saba:

Amina ninakuuliza, umesoma shule gani x2
Hukupata mimba, umekula kidonge gani,

*Kiitikio*:
Umewahanithi, Amina umewahanithi,
Laiti ungepata mimba, mtaani ingekuwa hadithi

Kama ilivyo kwa maeneo mengi ya hapa Tanzania, maeneo ya ukanda wa Pwani pia, kumekuwa na ongezeko kubwa la shule za msingi na sekondari ambazo zimeongeza fursa kwa watoto wa kike kuendelea na masomo yao ukilinganisha na miaka iliyopita. Hili pia limechagizwa na mkazo toka katika vyombo vya dola, taasisi za kiserikali na za watu binafsi kuhakikisha kuwa kila aliyepata nafasi hiyo anaitumia vema. Pamoja na kuwepo kwa hali hiyo, utafiti huu umebaini kuwa bado jamii hii inakabiliwa na changamoto ambazo tunaweza kuziita ni changamoto za watoto wa

kike kuonekana kuwa hawana haki ya kwenda shule au kukosa uwezo wa kuvumilia masomo bila kupata matatizo mbalimbali likiwemo suala la mimba.

Maudhui ya wimbo huu yanawalenga watu wote ambao bado hawaamini kama msichana wa Kizaramo anaweza kusoma kwa uhuru bila kupata mimba. Watu hao wamekuwa wakitoa maneno mengi ya kebehi na dharau pindi tukio la kupata mimba kwa mtoto wa kike linapotokea. Lakini watu haohao pia hupigwa na butwaa wanapoona kuwa jambo wanaloliwaza si la msingi na halina mashiko kwa jamii. Katika mistari miwili ya kwanza, mwimbaji anauliza maswali chochezi kwa Amina. Haya aliyauliza mbele ya hadhira ili kupiga vijembe dhidi ya watu wenye tabia kama hizo.

Ufutuhi katika wimbo huu unajipambanua wazi katika kiitikio cha wimbo huu. Huu unajengwa na maneno ya kuwakejeli watu hao kwa kutumia neno kali la “kuwahanithi”. Katika hali halisi, kuhanithi ni kitendo cha kuondoa uwezo wa kufanya mapenzi kwa binadamu mwenye jinsi ya kiume. Neno hili pia, hutumiwa kama “kuhasi”, kwa wanyama wengine wasio binadamu. Hili huibua hali ya ucheshi kwa hadhira kwa sababu, kitendo hiki hakina uhusiano wowote na masuala ya kumsema vibaya mtoto wa kike kulingana na maudhui ya wimbo huu. Aidha, kiitikio cha wimbo huu kinabainisha kijembe ambacho kinaelekezwa moja kwa moja kwa watu ambao walikuwa wakisubiri kumwona msichana huyo akishindwa kuendelea na masomo ili waweze kusema. Kijembe hiki kinaibua ucheshi kwa hadhira kutokana na fikra zao kujenga taswira ya mtu hanithi ili kupata sifa za watu waliokuwa wakimsema vibaya binti huyo. Kinalenga kuijuza hadhira kuwa kitendo cha Amina kutopata mimba kama walivyodhani ni cha aibu kwao.

Kwa jumla, wimbo huu unahalisika. Umemtaja Amina ambaye ndiye msichana aliyekuwa akifanyiwa unyago, na kufafanua maudhui ambayo yanasawiri maneno ambayo yalikuwa yakisemwa mara kwa mara katika wakati wote ambao Amina alikuwa akiendelea na masomo yake ya sekondari. Suala hili si kwa Amina tu, bali hujitokeza katika maeneo mengi ya jamii hii.

r) Wimbo wa Kumi na Nane:

Nipo barazani kwangu, maneno nimeyasikia, x2
Eti huyo Bi. Hindu, kutwa kucha kiguu na njia,

*Kiitikio*:
Chukua shoka, Kitumbi ukakate mkaa,
Bi Hindu analima, mipango itakaa sawa.

Wimbo huu pia huimbwa katika muktadha wa unyago hususani pale mtunzi anapodhamiria kufikisha hisia zake kwa mmojawapo kati ya watu waliokusanyika mahali hapo. Ndani ya jamii ya Wazaramo zipo kero kuu za umbea, majungu na fitina ambazo zimezoeleka kusikika masikioni mwa watu. Kero hizo zimekuwa zikibeba dhamira nyingi katika nyimbo za sherehe za unyago. Tungo za kifutuhi zinajipambanua wazi katika wimbo huu kwa lengo la kukemea vikali vitendo hivyo ambavyo ni vya ukweli na vimekuwa vikizua mijadala mingi ndani ya jamii. Baadhi ya wanajamii wamekuwa na tabia ya kujenga chuki dhidi ya wenzao wanaofanya jambo lolote, liwe baya ama zuri, na hata kama ni kwa faida yake au jamii nzima. Jina la Bi. Hindu limetajwa kisanaa ili kuibua fikra na ucheshi kwa hadhira kutokana na uhalisia wa kuwepo kwa mtu huyu na sifa zake ambazo hufahamika na wengi. Huyu ni mwigizaji maarufu na kwa sasa ni mtangazaji wa kipindi cha ‘Mitikisiko ya Pwani’ kinachorushwa na kituo cha redio cha *“Times FM”*. Kipindi hicho hupiga na kuchambua nyimbo za taarabu za kisasa (mipasho), zenye sifa sawa na nyimbo za Wazaramo. Mstari wa pili wa wimbo huu usemao “Eti huyo Bi Hindu, kutwa kucha kiguu na njia’ ni kijembe. Kutokana na hali iliyoonekana uwandani pamoja na

maelezo ya baadhi ya wanajamii, imebainika kuwa tungo hii si kauli halisi ya mtunzi, bali imetumiwa kama mwangwi wa kauli nyingi za kebehi kutoka kwa wanajamii wengine wanaomsema vibaya kuwa ni mtu wa kuzurura mitaani muda wote.

Aidha, kiitikio cha wimbo huu pia kimetaja jina halisi linalotambuliwa na hadhira ili kubeba dhamira za mwimbaji katika hali ya unyume. Kimetumika kama ni kijembe kwa mtu au watu hao ambao wamekuwa wakimwandama kwa maneno mwenzao huyo kwa kumwita mzururaji wakati akihangaika kujishughulisha na kazi mbalimbali za kiuchumi.

s) Wimbo wa Kumi na Tisa**:**

Mwenzenu ninauliza, mahala hapa pawaje x2?
Wananambia mpula mbatata, mdevu uumbikaje?

Wimbo huu ni mfupi; umeundwa na mistari miwili tu iliyosheheni tungo za kifutuhi kutoka kwa mtunzi wake. Tungo za wimbo huu zimechochea ucheshi na shamrashamra za watu hususani wale wanaojijua kuwa hawahusiki na dhamira lengwa ya wimbo huu. Mstari wa kwanza ambao upo katika mtindo wa swali ndio unaowezesha kuubaini ufutuhi uliopo katika mstari wa pili. Neno “mpula mbatata” ambalo maana yake ni pua kama mbatata limetumiwa na mwimbaji kibalagha kwa kuwa linajaribu kutia msisitizo kuhusu maumbile na mwonekano wa pua ya mtu kwa kuilinganisha na kiazi maarufu kama mbatata. Hali ya ucheshi katika tungo hii inajitokeza kutokana na ukweli kwamba, pua ya mtunzi huyu ni kubwa; na hivyo kuwafanya watu wailinganishe na kiazi. Hiki ni kijembe kilichopigwa kwa mtu au kundi la watu wenye tabia ya kutoa maneno ya dhihaka kuhusu maumbile ya watu wengine. Kwa njia ya sanaa ya nyimbo na kwa kutumia muktadha wa sherehe hizi

kama jukwaa la malumbano, mtunzi ambaye ndiye aliyedhihakiwa hapo awali kuhusu pua yake, anajaribu kujibu vijembe vya adui yake huyo kwa kupitia swali analoiuliza hadhira kuwa “mdevu uumbikaje?”; yaani, kidevu chake kimeumbikaje?

Kutokana na ufafanuzi wa mtunzi, kauli za kupigana vijembe kuhusu maumbile yao ni halisi na zilikuwepo kwa muda mrefu. Hivyo, lengo lake hapa lilikuwa ni kuitaka hadhira ijaribu kulinganisha umbo baya la pua yake pamoja na kidevu kibaya cha adui yake; na hatimaye, waamue ni yupi anastahili kupewa sifa mbaya. Wimbo huu huimbwa wakati pande hizo mbili zinazohasimiana zikiwa ni sehemu ya hadhira iliyokusanyika katika sherehe za unyago wa Wazaramo.

t) Wimbo wa Ishirini:

Kwa mama Amina siendi miee, eee siendi miee, x2
Kanipikia mihogo, mihogo ina mizizi,
Ana roho mbaya, umuone hivihivi.

Huu ni wimbo wa unyago ambao pia, umetungwa kwa kufuata kaida za kifutuhi. Dhamira kuu ya wimbo huu ilikuwa ni kukemea vikali tabia za roho mbaya ambazo baadhi ya watu ndani ya jamii huwa nazo. Tabia hizo zinakemewa kwa kutumia kauli ambazo zinaweza kuonekana kuwa ni kali masikioni, lakini ndizo zibebazo mawazo ya msingi ya mtunzi. Kwa mfano, katika mstari wa kwanza imeonekana namna msisitizo unaowekwa kuhusu kutokwenda kwa Mama Amina. Jina hili ni halisi na linahalisika kwa kuwa ametajwa mtu maarufu hasa katika sherehe hiyo ya unyago iliyokuwa ikifanyika katika mahali hapo. Kwa jumla, mistari yote mitatu ya wimbo huu imebuniwa kisanaa ili kupiga kijembe kwa watu wote wenye tabia ya ubinafsi; ya kutopenda wageni katika miji au familia zao, na si mama Amina aliyetajwa kwenye tungo zake. Aidha, vijembe hivi pia vinaweza kumhusu mtoto wa

kike anayechezwa unyago, kwa kuwa tayari amebalehe na kuwa tayari kuolewa na kuanzisha familia yake. Tafsiri ya wimbo huu iliyopatikana ni kuwa, siku zote mji au familia yoyote haikosi wageni. Kuendelea kwenda au kutokwenda kwa wageni hao katika familiya hiyo hutegemea namna ambavyo watakuwa wakipokelewa ama kwa furaha na unyenyekevu au kupokelewa kwa chuki na manung'uniko kutoka kwa mwenyeji wao.

Hakuna tatizo kwa mtu yeyote kupika au kupikiwa mihogo katika jamii ya Wazaramo kwa kuwa hiki ndicho chakula kikuu ambacho kinapatikana sana katika ukanda wao. Katika wimbo huu, chakula hiki kimedunishwa na kupewa hadhi ya chini ili kukidhi haja ya mtunzi kulimulika suala hilo kwa jicho pevu huku akitumia sanaa ya ufutuhi kama kibebeo cha dhamira zake.

Kutokana na mjadala huo kuhusu nyimbo za sherehe za unyago katika jamii ya Wazaramo, ni wazi kuwa dhana za kejeli, vijembe, dhihaka na balagha ambazo kwa pamoja zinaunda dhana msingi ya ufutuhi, ndizo hasa hutumiwa katika nyimbo nyingi za Wazaramo. Sehemu kubwa ya tungo zitumikazo huwa na maana za msingi za kifasihi, ambapo maana hizo ndizo hubeba dhamira za nyimbo hizo.

### 4.4 Dhima za Ufutuhi katika Nyimbo za Sherehe za Unyago wa Wazaramo

Imebainika kuwa matumizi ya tungo za kifutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo ni jambo lisiloepukika. Hii ni kwa sababu, sanaa hii ina muda mrefu katika historia ya jamii hii. Kila tungo itumikayo huwa na lengo, si tu la kuburudisha, bali kubeba wazo la msingi la mtunzi au mwimbaji. Lengo la msingi la kutumika kwa tungo hizi ni kujaribu kuyaakisi matukio mbalimbali yatokeayo ndani

ya jamii na kuyasema kwa wanajamii wengine kwa njia hiyo iliyojaa vijembe, kejeli, dhihaka, ubeuzi na balagha nyingi. Matukio yanayoakisiwa katika nyimbo hizo ni yale yanayofungamana na mfumo wa maisha ambao jamii ya Wazaramo imejikuta ikiutumia katika maisha yao ya kila siku. Ufutuhi katika nyimbo hizi hutumiwa kwa malengo mahususi ambayo husaidia kubeba dhamira za msingi za wimbo husika. Kwa jumla, utafiti umebaini kuwa tungo za kifutuhi zitumikazo katika nyimbo za unyago wa Wazaramo, zimekuwa na dhima zifuatazo kwa hadhira:

### 4.4.1 Kudokeza Mawazo Mazito ya Mwimbaji kwa Hadhira

Katika mjadala wa matokeo ya utafiti, imebainika kuwa kila wimbo uimbwao katika sherehe za unyago wa Wazaramo hutawaliwa na hisia zinazomfanya mtu atunge au aimbe. Ni kutokana na hisia hizo, watunzi wa nyimbo huamua kutumia vijenzi vya kifutuhi ili kurahisisha malengo hayo. Vijenzi hivyo ndivyo hupachikwa na kubebeshwa mawazo ya msingi ambayo mwimbaji amedhamiria kuyafikisha kwa hadhira iliyopo. Aidha, mawazo hayo ndiyo huibua dhamira za mwimbaji ambazo zinaweza kumlenga mwali wa Kizaramo au washiriki wengine waliojumuika katika mkusanyiko huo. Hisia hizo zinaweza kuwa ni za furaha au huzuni kutegemeana na matukio mbalimbali yaliyotokea ama yanayotokea katika jamii yao. Waimbaji huweza kuimba wao wenyewe na dhamira za nyimbo zao kuifikia hadhira iliyokusanyika moja kwa moja au wakati mwingine utaratibu wa kuimbiana (kuimba badala ya mtu mwingine) hufanyika.

Mbinu za kifutuhi zenye ucheshi na unyume wa kimaana ndizo hutumika kubeba mawazo hayo. Kwa mfano, mwimbaji anaweza kulalamika kuhusu hali ya umasikini aliyonayo wakati katika uhalisia ameweza kuandaa sherehe hiyo na kuwafanya watu

waweze kula, kunywa na kucheza kwa furaha. Wakati mwingine mwimbaji anaweza kutumia jina la mtu mwingine katika tungo za wimbo wake, na hata kumnyooshea mtu kidole wakati wa kuimba lakini mawazo ya mwimbaji yaliyofinyangwa ndani ya wimbo huo yakilenga kumfikia mtu tofauti aliyepo miongoni mwa hadhira iliyokusanyika. Mfano wa hali hii twaweza kuiona katika wimbo wa kumi na nne.

### 4.4.2 Sanaa ya Kufunda Mwali wa Kizaramo

Katika baadhi ya nyimbo zilizoshughulikiwa katika utafiti huu, waimbaji wametumia tungo mbalimbali za kifutuhi ambazo zimelenga kubeba dhima tofauti za kuwafunda watoto wa kike ambao wanachezwa unyago. Tungo bunilizi za kifutuhi hufinyangwa kisanaa kwa kuweka wazi matukio halisi ambayo yanaweza kumkabili msichana wa Kizaramo pindi atakapoyaanza maisha yake ya kiutu uzima. Miongoni mwa mafundisho yatolewayo kwa mtoto wa kike kupitia tungo za kifutuhi ni haya yafuatayo:

Mosi, msichana wa Kizaramo anapopelekwa unyagoni ni ishara ya kuwa tayari anao uwezo wa kuyaanza maisha ya utu uzima. Hivyo, mafundisho kuhusu maisha mapya ya ndoa hutolewa kwake bila kujali kama msichana huyo ameshapata mchumba ama bado. Kwa kutumia sanaa ya kifutuhi, watunzi na watambaji hulimulika suala hili kwa jicho pevu kwa kuamini kwamba ndoa ni tukio zito na hatua muhimu ya kimaisha inayohitaji mtu aliyepevuka na kuandaliwa kifikra kabla ya kulizamia. Mojawapo ya vikwazo ambavyo huwapata mabinti walio katika ndoa ni kuongezeka kwa marafiki maarufu kama “mashoga” ambao huaminika kuwa ni chanzo kimojawapo cha kuyumba kwa ndoa nyingi. Baadhi ya marafiki hao huwa na tabia ya kuchonganisha watu na wakati mwingine kubuni kauli za kichochezi ambazo

husababisha mipasuko katika ndoa nyingi. Tungo za kifutuhi zinazowasuta watu wenye tabia kama hizo hulenga kuwajenga kifikra watoto wa kike juu ya kuchukua tahadhari za mapema pindi watakapokutana na changamoto hizo za kimaisha.

Pili, wasichana wanapovunja ungo huambatana na mabadiliko mbalimbali ya kimwili na kitabia. Mabadiliko hayo yanaweza kuwa ni yenye tija au kuibua kero na usumbufu kwa jamii yake. Baadhi ya wasichana wanaopata bahati ya kufundwa hutumia mafundo hayo vizuri kwa manufaa mazuri kwao binafsi na jamii zao kama vile usafi binafsi, juhudi katika kazi, malezi, pamoja na kuheshimu watu wote. Utafiti umebaini kuwepo kwa malalamiko toka kwa baadhi ya wanajamii kuhusu tabia mbaya ambazo hujijenga mara baada ya tukio la unyago kufanyika. Baadhi ya wasichana hao hukosa adabu na kuanza kutenda mambo mengi mabaya sambamba na kujihusisha katika mapenzi kwa pupa, kutokana na kujengeka kwa hali ya kujiamini kupita kiasi kuwa, tayari wao ni watu wazima na wana uhuru wa kuamua yale wanayojisikia kuyafanya. Katika baadhi ya nyimbo zilizokusanywa na kuchambuliwa katika utafiti huu, imebainika kuwepo kwa tungo nyingi za kifutuhi zinazoweza kumsuta mwali wa kizaramo juu ya tabia mbaya ambazo hapaswi kujihusisha nazo, likiwepo suala la kutojiheshimu yeye pamoja na kutoheshimu watu wengine.

### 4.4.3 Nyenzo ya Kuendeleza Usemezano

Jamii ya Wazaramo kama zilivyo jamii nyingine za Kitanzania imekuwa ikikabiliwa na uhasama na migogoro midogomidogo ya kijamii baina ya pande mbili. Hali hiyo husababisha kuwepo kwa malumbano ambayo huweza kuonekana wazi au katika hali fiche. Wakati mwingine, pande hizo mbili na hasimu hufikia hatua ya

kukabiliana ana kwa ana kwa njia ya maneno au matendo huku kila mmoja akitoa hisia zake za chuki au kukerwa na jambo fulani toka kwa mwingine. Malumbano na uhasama mwingine huweza kuibuliwa na kuendelezwa kupitia tungo mbalimbali za kifutuhi, ambapo hadhira iliyokusanyika hupata fursa ya kushuhudia na kusikia malumbano hayo kwa kupitia sanaa hiyo iliyojaa ucheshi na tafakari nyingi. Hivyo, Wazaramo hutumia muktadha huo ili kutoa maneno ya kukejeli, kudhihaki au kuwapiga vijembe watu wengine kulingana na vile wanavyojisikia kufanya ilimradi nafsi zao ziweze kuridhika. Hali kadhalika, kauli hizo zinaweza kupata upinzani wa majibu kutoka kwa mwimbaji mwingine aliyeguswa na kauli hizo na kuufanya uwanja huo wa unyago kuwa kama jukwaa la marumbano ya watu kwa kutumia kauli za kifutuhi.

### 4.4.4 Sanaa ya Kuburudisha Hadhira

Sifa kuu ya tungo za kifutuhi ni uwezo wake katika kuibua ucheshi huku ukiiacha hadhira kuwa katika tafakari nyingi kuhusu dhamira za tungo hizo. Wakati mwingine, tungo za kifutuhi katika nyimbo hizo hudhamiria kuburudisha hadhira na kuwafanya wawe na furaha kutokana na ufundi wa kufinyanga maneno sambamba na matendo yafanywayo na waimbaji wa nyimbo hizo. Mtindo wa majibizano ya maneno kwa njia ya nyimbo zilizotawaliwa na viashiria vya kifutuhi kama vile vijembe, dhihaka, kejeli na balagha, hukamilisha furaha ya hadhira na kuwafanya watu wengi kupenda kuhudhuria katika sherehe hizo kila zinapofanyika. Hali ya watu kuishia kuburudika na tungo za kifutuhi wakati mwingine husababishwa na kuwepo kwa tofauti za umri, jinsia, elimu, na uelewa wa utamaduni wa jamii hii. Kuwepo kwa tofauti hizi huwafanya baadhi ya watu

kupitwa na maudhui ya tungo hizo na hivyo kubakia kuwa washiriki ambao wanafurahia maneno au matukio yatendekeyo katika muktadha huo.

### 4.4.5 Kitambulisho cha Jamii ya Wazaramo

Matumizi ya tungo hizi kwa Wazaramo yana upekee wake miongoni mwa jamii nyingi za Kitanzania. Kila jamii iliyopo nchini huwa na sifa zake pambanuzi ambazo zaweza kuitofautisha na jamii nyingine. Sifa hizi zaweza kujigawa katika misingi mbalimbali ya kimaisha kama vile uchumi wao, siasa zao, na utamaduni wao. Kwa mfano jamii ya wamasai hujipambanua vema kutokana na utamaduni wao wa kulipenda vazi lao la asili. Hivyo, kuifanya jamii hii kulitumia vazi hili ili kudhihirisha uwepo wao. Halikadhalika Wazaramo nao wana sifa kubwa ya kupenda kutumia tungo hizi popote walipo ili kuutambulisha Uzaramo wao. Kwa upande wao, tungo hizi huzitumia si kwenye kuimba tu bali hata katika mazungumzo ya kawaida. Ni jamii inayopenda kuzungumza chochote kilichopo ndani ya nafsi ya msemaji ilimradi hisia zake zisikike mbele za watu. Ndiyo mana wakati mwingine tungo za nyimbo zao hutawaliwa na kauli za matusi na uchochezi, ambazo pia hufichama ndani ya tungo za kifutuhi ili kuibua maudhui ya mtunzi. Sifa hizi zote ndizo huweza kuitofautisha jamii hii na jamii nyingine za Kitanzania.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imejadili matokeo ya uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka uwandani na maktabani. Mjadala umegawanywa katika sehemu tatu. Mambo ya msingi yaliyojadiliwa katika sehemu hizo ni; miktadha inayowasukuma Wazaramo kutumia tungo za kifutuhi wakati wa sherehe za unyago, tungo za kifutuhi zilizopo katika

nyimbo za Wazaramo, na mwisho, dhima mbalimbali za ufutuhi huo kwa hadhira zimejadiliwa.

Vijenzi vya ufutuhi kwa mfano, vijembe, kejeli, dhihaka na balagha ambavyo vimechambuliwa kwa pamoja katika sura hii vimeonekana kuwa na nafasi kubwa ya kubeba dhima mbalimbali kwa hadhira kwa kuwa vimetawaliwa na hali ya ucheshi unaowafanya watu wayapate maudhui ya nyimbo kwa njia ya burudani. Pia, njia hii imeonekana kuwa bora katika kubeba ujumbe wa waimbaji kwa kuwa hujenga kumbukumbu ya muda mrefu kwa hadhira inayoshiriki tukio hilo. Hivyo, mjadala huu umewezesha kuibua mapendekezo ya jumla ambayo yataweza kuwasaidia wanataaluma na watafiti wajao katika kuziboresha tafiti zao. Mapendekezo hayo yamefafanuliwa zaidi katika sura inayofuata.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inadokeza masuala muhimu; nayo ni muhtasari wa tasnifu, hitimisho, na mapendekezo kwa tafiti zijazo. Mambo hayo ndiyo yanayounda sehemu muhimu za sura hii.

## 5.2 Muhtahsari wa Tasnifu

Mada ya utafiti huu ilihusu kuchunguza ‘Ufutuhi katika Nyimbo za Sherehe za Unyago wa Wazaramo; Utumizi na Dhima Zake kwa Hadhira’. Tasnifu imebainisha jinsi ambavyo jamii ya Wazaramo inaweza kutumia vijenzi vya ufutuhi katika kubeba dhima mbalimbali kwa hadhira na kufafanua mambo mbalimbali yanayojiri katika jamii kulingana na mfumo wa maisha uliopo. Tasnifu hii ina sura tano; na kwa ufupi, yafuatayo ni maelezo ya kila sura:

Sura ya kwanza inatoa dira ya utafiti. Katika sura hii, dhana ya ufutuhi na vijenzi vyake ilipatiwa ufafanuzi wa kutosha. Vile vile, ilifafanua historia fupi ya jamii ya Wazaramo katika vipengele vya eneo la kijiografia, shughuli za kiuchumi pamoja na lugha. Pia, sura hii imefafanua kuhusu usuli wa tatizo la utafiti. Hapa, ufafanuzi wa kina kuhusu sherehe za unyago katika jamii ya Wazaramo umetolewa ili kuweza kutoa mwongozo mzuri katika kuutazama ufutuhi na namna unavyoweza kutumika katika sherehe hizo kwa malengo mbalimbali. Aidha, yameelezwa masuala yahusuyo tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, na mwisho ni nadharia iliyotumika katika utafiti huu.

Sura ya pili ilijikita katika ufafanuzi wa maandiko mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu. Maandiko hayo yalitoa msaada mkubwa katika mchakato wa ubainishaji wa mapengo mbalimbali yaliyojitokeza katika machapisho na tafiti tangulizi zilizozipitiwa na hatimaye kutoa fursa ya kulizamia suala la ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo. Sura ya tatu imeelezea mbinu na vifaa vilivyotumika mpaka kukamilika kwa utafiti huu. Sura hii imebainisha mpango mzima wa utafiti ulivyokuwa, aina ya kundi lililohitajika katika kutoa majawabu ya maswali ya utafiti pamoja na namna data zilivyokusanywa na kuchambuliwa kulingana na mwongozo wa nadharia iliyochaguliwa kutumika. Nadharia ya Uhalisia ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data za utaifiti huu kwa kuzingatia misingi yake mikuu miwili ya kuyatazama mambo. Misingi hiyo ni uhalisia kama namna ya kutathmini hali ikihusisha uhalisia wa maisha ya watu. Mwingine ni ule unaoihusisha na kazi ya sanaa inayoonesha namna maisha ya binadamu jinsi yalivyo, kwa kuhusianisha na uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu kwa kutumia mbinu za kisanaa. Maeneo muhimu yaliyojumuishwa katika sura hii ni mpango wa utafiti, mahali pa utafiti, mbinu ya utafiti, njia na zana za ukusanyaji wa data, walengwa wa utafiti, uchambuzi wa utafiti, pamoja na vikwazo mbalimbali vilivyojitokeza katika mchakato wa ukamilishaji wa utafiti.

Sura ya nne imejadili matokeo ya utafiti. Sura hii imepangwa katika sehemu kuu tatu, ambazo kwa pamoja zinajibu maswali matatu yanayoulizwa katika utafiti huu. Sehemu ya kwanza imejadili miktadha inayowafanya Wazaramo watumie tungo za kifutuhi katika nyimbo zao. Sehemu ya pili imebainisha na kufafanua tungo za kifutuhi zilizopo katika nyimbo za unyago wa Wazaramo; na sehemu ya tatu imefafanua dhima za ujumla za matumizi ya tungo za kifutuhi kwa hadhira.

Sura ya tano imetoa muhtahsari wa utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni muhtahsari wa tasnifu, utoshelevu wa nadharia katika uchambuzi wa data, matokeo ya utafiti, mambo ya kuzingatia ili kuepukana na changamoto, pamoja na mapendekezo kwa watafiti wajao, kuyazamia masuala ya unyago sambamba na sanaa ya nyimbo hizo katika kuyasawiri matukio yaliyopo kwa ujumla wake. Mwisho, hitimisho la jumla limetolewa.

### 5.3 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika

Katika utafiti huu, nadharia ya Uhalisia ndiyo iliyotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti. Vipengele vya nadharia hii vimejiegemeza katika dhana kuu mbili. Dhana ya kwanza ni ile inayoitazama nadharia hii kama njia ya kutathmini hali, yaani uhalisi katika mfumo mzima wa maisha ambao jamii inaufuata. Dhana ya pili ni ile inayoitazama nadharia hii kama kazi ya sanaa inayoonesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo kwa kuhusianisha na uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu kwa kutumia mbinu za kisanaa. Vipengele vya nadharia hii vimetusaidia katika kung'amua kuwa ufutuhi ni ufundi wa kisanaa ndani ya sanaa kuu ya uimbaji katika sherehe za unyago. Nadharia hii pia, imewezesha kubaini kuwa tungo bunilizi zote za kifutuhi zitumikazo katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo hulenga katika kuweka wazi hisia za ndani za mwimbaji ambazo, kwa kiasi kikubwa, ni zile zitokanazo na matukio halisi yatokeayo kwake ama kwa wanajamii wengine, na kumfikia kwa njia ya kushuhudia au kusikia yakitendeka. Hivyo, nadharia hiyo imefaa katika kuzitafiti tungo za kifutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo na kubaini dhima zake kwa hadhira.

### 5.4 Mambo Mapya Yanayoibuliwa na Tasnifu Hii

Mambo mapya yaliyomo katika tasnifu hii ni:-

Kwanza, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa sehemu kubwa ya nyimbo ziimbwazo katika sherehe za unyago wa Wazaramo zimetawaliwa na misingi ya kifutuhi. Watunzi na waimbaji wa nyimbo hizo hutumia tungo hizo ili kuyamulika masuala ya kila siku yanayowazunguka katika jamii zao. Mbinu hiyo ya kisanaa ya ufikishaji ujumbe huzua mabishano na majibizano endelevu kati ya mtu na mtu au kundi fulani lenye kuwa na urafiki wa karibu dhidi ya kundi lingine. Ni jambo la kawaida kukuta mwimbaji mmoja akitunga na kuimba wimbo mahususi kwa lengo la kumjibu mwimbaji mwingine aliyetangulia. Hapo ndipo baadhi ya tungo za kifutuhi kama vile vijembe na kejeli hutumika kiufundi ili kukidhi haja za waimbaji hao. Kutokana na hali hiyo, kusudio la msingi la kufanyika kwa sherehe za unyago, ambalo ni kumfunda na kumuandaa msichana wa kizaramo kuyakabili maisha mapya ya kiutu uzima, limekuwa likipoteza dira yake kwani wanajamii hutumia muda mwingi kupeana mipasho kutokana na mambo kuhusu masuala ya kijamii yanayojiri kila siku.

Pili, utafiti umebaini kuwa utamaduni wa kuimba nyimbo katika sherehe za unyago bado upo, lakini umekuwa ukitofautiana kati ya ukoo mmoja na mwingine. Kumekuwa na kawaida kwa Wazaramo kutunga nyimbo mpya ambazo huendana na wakati sambamba na matukio anuai yanayojiri kwa wakati huo. Jambo hili limesababisha kukosekana kwa nyimbo za aina moja zinazoimbwa katika jamii yote ya Wazaramo. Nyimbo zote zilizochambuliwa katika utafiti huu zilikuwa na vijenzi

vyake vya kifutuhi ambavyo vililenga kubeba ujumbe uliodhamiriwa na waimbaji kuifikia hadhira yao.

Tatu, kuna uwiano mkubwa kati ya fani ya nyimbo za sherehe za unyago ziimbwazo katika jamii ya sasa ya Wazaramo, pamoja na fani ya kazi nyingine za Fasihi Simulizi mfano muziki wa taarabu za kisasa maarufu kama mipasho na muziki wa kizazi kipya maarufu kama 'Bongo Fleva'. Sanaa hizi zote kwa sasa zimetawaliwa na mtindo wa kurushiana maneno makali ambapo pande mbili hujibizana kisanaa kwa kutumia tungo mbalimbali za kifutuhi ambazo ndizo huchopekwa ujumbe wa waimbaji kwa maneno yenye viashiria vya kejeli, dhihaka, vijembe ama balagha ili kuweka wazi hisia za waimbaji zinazohusiana moja kwa moja na uhalisia wa matukio na mfumo wa maisha wanamoishi.

Nne, utafiti umebaini kuwa utamaduni wa kufanyika kwa sherehe za unyago katika jamii ya Wazaramo bado upo katika baadhi ya koo ijapokuwa kasi yake imekuwa ikipungua siku baada ya siku. Kupungua kwa kasi huko kunasababishwa na sababu kadha wa kadha ikiwapo ugumu wa maisha unaotokana na kipato duni miongoni mwa wanajamii pamoja na kuongezeka kwa fursa za watoto wa kike kuendelezwa katika elimu hususani elimu ya sekondari. Hili linawafanya watoto wengi kushindwa kuwekwa ndani kwa muda mrefu kwa ajili ya kufanyiwa mila za unyago, kutokana na kuhudhuria shughuli za kimasomo.

Mwisho, ni kutokana na kuibuka kwa sanaa mpya ya burudani iitwayo kwa majina maarufu kama "rusha roho", au "kigodoro", ambayo kwa kiasi kikubwa, jamii ya Wazaramo imekuwa ikiitumia kwa ajili ya kufanyia sherehe zao za unyago. Katika

sanaa hii ya kisasa ya utoaji burudani, muziki wa taarabu za kisasa hutumiwa sambamba na mirindimo ya muziki utumiao vyombo vya kisasa kama vile gita, vinanda, ngoma na matarumbeta. Mtindo huu ni mpya na unafifisha utaratibu mzima wa unyago uliokuwa ukifanyika awali. Hii ni kwa sababu katika sanaa hii binti wa Kizaramo huwa hawekwi ndani kwa kipindi kirefu na utumbuizaji wake si wa moja kwa moja kati ya waimbaji na hadhira, bali hutegemea nyimbo zilizorekodiwa na kuhifadhiwa kwenye vifaa maalumu kama vile CD na vinyonyeo.

### 5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Kukamilika kwa tasnifu hii hakumaanishi kuwa mambo yote yahusuyo nyimbo na utamaduni wa unyago yamejumuishwa katika mada hii. Mchakato wa ukusanyaji na uchambuzi wa data ulizingatia malengo na maswali yaliyokidhi haja za utafiti huu pekee. Kwa sababu hiyo, hapa yanatolewa mapendekezo na maoni ya jumla juu ya watafiti zaidi kujielekeza katika kuzipigia mbizi kona nyingine za fasihi hii simulizi ihusuyo nyimbo za sherehe za unyago. Ufafanuzi kuhusu mapendekezo kwa ajili ya tafiti zijazo unatolewa kama ifuatavyo:

Mafundo ya unyago kwa watoto wa kike bado yana dhima na thamani kubwa kwa jamii ya sasa. Hii ni kwa sababu huwajengea uwezo wa kifikra ili kukabiliana na changamoto za kimaisha pindi wanapoyaanza maisha mapya ya kiutu uzima, hususani, maisha ya ndoa. Pamoja na thamani hiyo, ni wazi kuwa utamaduni huo kwa sasa umekuwa ukikabiliwa na changamoto za kupoteza sifa na mabadiliko katika mfumo mzima wa uendeshaji wa tukio hilo la kimila. Hapa, mtafiti anapendekeza kuwepo kwa tafiti za ziada ambazo zitajikita katika kuchambua

mabadiliko ya kijamii na athari zake katika sherehe za unyago za makabila mbalimbali ya Tanzania.

Pia, kutokana na mambo ambayo yalishuhudiwa uwandani, mtafiti anapendekeza kuwepo kwa tafiti nyingi ili kuchambua mabadiliko ya kimaudhui katika nyimbo za sherehe za unyago katika makabila ya Tanzania, likiwapo kabila la Wazaramo. Hii ni kwa sababu nyimbo nyingi zimeonekana kupoteza lengo lake la msingi ambalo ni kumfunda msichana wa Kizaramo kwa njia ya burudani. Baadhi yazo zimekuwa zikitumika kama silaha ya malumbano na majibizano kati ya wanajamii wenyewe.

Mwisho kabisa, utafiti huu umeshughulikia suala la ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo. Mtafiti anapendekeza tafiti zaidi zifanywe katika maeneo mbalimbali kuhusu fani nyingine za nyimbo za unyago kwa kuzungukia vipengele vya muundo, mtindo na vipengele vingine vya lugha mfano tamathali za semi.

## MAREJELEO


Adewole, S.M (1984), "Agreement as a Cohesive Device in Kiswahili", M.A Dissertation, University of Dar es Salaam: Tanzania, (Haijachapiswa).

Bakari, H. (2011), "Athari za Nyimbo za jando na Unyago za Wamakuwa kwa Vijana" Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma: Tanzania, (Haijachapishwa).

Balisidya, M.L (1989), "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi", Mulika namba 19:2-10. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Finnegan, R. (1984), *Oral Literature*, Africa. Oxford University Press.

Kenyata, F.A. (1999), *Malezi na Sala katika Kabila la Kimatengo*, Benedictine Publications: Ndanda-Peramiho.

Khatib, M.S. (1978), "Vitendawili- Fani ya Fasihi Simulizi". Katika *Mulika* toleo namba 13: uk21", Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kothari, C.R. (2004), *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Age International (P) Limited Publishers: New Delhi.

Madumulla, J.S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili, Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Mture Educational Publishers: Dar es Salaam.

Mahundi, S. (2012), "Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Sherehe za Jando na Unyago; Jamii ya Wamwera", Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaaam: Tanzania, (Haijachapishwa).

Mauya, A.B. (2006), *Semi: Maana na Matumizi*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mazigwa, S.A. (1991), *Fasihi ya Kiswahili*, Ndanda Mission Press: Peramiho/ Ndanda.

Mfaume, R.R. (2013), Malenga wa Milenia (2): Kivuli Kiamboni, Luhimba Publishers: Morogoro.

Muhando, P na Balisidya, N. (1976), *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*, Tanzania Publishing House: Dar es Salaam.

Mission ya Kievangelishe, (1935), *Habari za Wazaramo*, Usambara Agentur, Mission ya Lwandai.

Mkumbugo, M. (2003), "Nyimbo za Unyago katika Kabila la Wasambaa", katika *Fasihi Simulizi: Nyimbo za Kumbi*, Taasisi za Kiswahili: ar es Salaam.

Mkunduge, G.L.M (1971), "Nyimbo za Kienyeji", katika *Kiswahili Fasihi na Ufanisi*, Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mlama, P. (1973), "Music in Tanzania: The Traditional Centre, The Kaguru as a Case Study". PhD Thesis, University of Dar es Salaam: Tanzania, (Haijachapishwa).

Mrope, R.A. na Mrope, D.A. (2001), *Historia ya Wamakuwa Kuhamia Tanzania kutoka Msumbiji*, Ndanda Mission Press: Peramiho.

Msokile, M. (1992), *Misingi ya Hadithi Fupi*, Dar es Salaam University Press: Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1989), "Tanzu za Fasihi Simulizi", Mulika Namba 21, TUKI: Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1996), *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar es Salaam.

Ntarangwi, M. (2004), "Uhakiki wa Kazi za Fasihi". PhD Thesisi, Augustana College: Rock Island.

Nunan, D. (1972), *Research Methodology in Lnguage Learning*, Cambridge University Press: Cambridge.

Okpewho, I. (1992), *African Oral Literature*, Indiana University: Bloomington.

Omari, C.K na Mvungi, M. (1981), *Urithi wa Utamaduni Wetu*, Tanzania Publishing House: Dar es Salaam.

Omari, S. (2009), "Tanzania Hip Hop Poetry as Popular Literature", PhD Thesis, University of Dar es Salaam: Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Ponera, A.S. (2010), "Athari za Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana, Matumizi na Athari Zake kwa Wasomaji", Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo kikuu cha Dodoma: Tanzania (Haijachapishwa).

Salinguji, N. (2011), "Nafasi ya Mwanamke katika Nyimbo za Wasukuma", Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma: Tanzania (Haijachapishwa).

Sengo, T.S.Y na Lucas, S.A. (1975), *Utani na Jamii: Ukwere*, Foundation Books Limited: Nairobi.

Senkoro, F.E.M.K. (1982), *Fasihi*, Press and Publicity Centre: Dar es Salaam.

Senkoro, F.E.M.K. (2007), "Lugha na Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki", CHAKAMA (Haijachapishwa).

Songoyi, E.M. (1988), "The Arts and The State of Tanzania: A Study of Two Singers, Kalikali and Mwinamila", M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam: Tanzania (Haijachapishwa).

Thonya, L.M. (1978), *Misingi ya Kiswahili*, Black Stars Agencies: Dar es Salaam.

Wafula, R, na Njogu, K. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*, Phoenix Publishing: Nairobi.

Wamitila, K.W. (2003), *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Focus Publications: Nairobi.

Wamitila, K.W. (2008), *Kazi za Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.

## VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO NAMBA '1'

## MWONGOZO WA MAHOJIANO KWA WAIMBAJI

i. Jina la mtafitiwa……

ii. Umri……..

iii. Jinsia…….

iv. Tarehe……...

v. Eneo/Mahali pa mahojiano……

1. Je, unazungumziaje kuhusu ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo?
2. Je, unaelewa nini kuhusu dhana zifuatazo?
    i. Kejeli……..
    ii. Dhihaka……..
    iii. Balagha……..
    iv. Vijembe……..
3. Je, unaweza kuimba wimbo wowote wa unyago unaoufahamu?
4. Wimbo uliouimba una maana gani kwa ujumla?
5. Je katika wimbo huu, kuna kejeli yoyote?
6. Kama jibu ni ndiyo, kejeli hiyo inamhusu nani?
7. Katika wimbo huu kuna kijembe chochote?
8. Kama jibu ni ndiyo, kijembe hicho kinamhusu nani?
9. Katika wimbo huu kuna balagha yoyote?
10. Kama jibu ni ndiyo, kwa nini umeamua kuitumia katika wimbo huu?
11. Katika wimbo huu kuna dhihaka yoyote?
12. Kama jibu ni ndiyo, dhihaka hiyo inamhusu nani?

13. Je, tungo hizi ulizozitumia katika wimbo/nyimbo zako zina dhima gani kwa hadhira hii?

Ahsante kwa ushirikiano wako.

**KIAMBATISHO NAMBA '2'**
**MWONGOZO WA MAHOJIANO KWA WASIKILIZAJI WA NYIMBO ZA SHEREHE ZA UNYAGO WA WAZARAMO**

i. Jina la mtafitiwa……

ii. Umri……..

iii. Jinsia…….

iv. Tarehe……...

v. Eneo/Mahali pa mahojiano……

1. Je, katika nyimbo za sherehe za unyago wa Wazaramo, kuna matumizi yoyote ya kejeli, vijembe, dhihaka au balagha?
2. Je, katika wimbo wowote uliousikia katika sherehe hizi, tungo zipi za kifutuhi zinajitokeza?
3. Kwa maoni yako, tungo hizi zina maana gani kwako wewe msikilizaji?
4. Je, unadhani ni kwa nini waimbaji wengi huamua kutumia maneno ya kifutuhi wakati wa kuimba nyimbo zao?
5. Je, matumizi ya maneno hayo ya kifutuhi yana dhima gani kwa upande wako?

Ahsante kwa ushirikiano wako.

**KIAMBATISHO NAMBA ‘3 ’: Picha za Sherehe za Unyago wa Wazaramo**




Kiambatisho 3‘a’: Mwali wa Kizaramo akisindikizwa na shangazi yake wakati wa sherehe ya unyago kijiji cha Kibamba, Februari 2014. (Chanzo: Mtafiti)




Kiambatisho 3’b’: Utamaduni wa kupeana zawadi wakati wa sherehe za unyago wa Wazaramo Kijiji cha Kibamba, Februari 2014. (Chanzo: Mtafiti)




Kiambatisho 3’c’: Wali wa Kizaramo wakiwa wamewekwa chini kwa ajili ya kupewa zawadi wakati wa sherehe za unyago kijiji cha Kibamba, Februari 2014. (Chanzo: Mtafiti)




Kiambatisho 3’d’: Wali wa Kizaramo wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa sherehe za unyago kijiji cha Kibamba, Februari 2014. (Chanzo: Mtafiti)